# Nipashe

Alhamisi Septemba 17, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580341

www.ippmedia.com

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710





UKURASA 11



## Kabudi aponda ripoti ya Umoja wa Mataifa uchaguzi Tanzania

UKURASA 2

# Mchuano wa sera wagombea urais

**JPM** atangaza kumaliza kero sugu 12, Lissu asema ruksa wakulima kuuza mazao popote, Lipumba ajinadi kuwakomboa wakulima wa tumbaku...

*Endelea Ukurasa wa 2, 3, 9*



## DK. MWINYI AITEKA PEMBA, AAHIDI KUFIKA KILA WILAYA

UKURASA 3

Mgombea urais wa Zanzibar kwa tiketi ya CCM, Dk. Hussein Mwinyi, akihutubia mkutano wa ufunguzi wa kampeni za uchaguzi mkuu katika uwanja wa Gombani ya Kale, Chakechake, Pemba jana. **PICHA: IKULU**

## AJALI YAUA WATU WATANO

UKURASA 5

**MICHEZO** ZLATKO: CARLINHOS BADO NI WA BENCHI YANGA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6


Fursa kwa Wagombea! 2020

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini

Je ungependa kukishukuru chama chako ?

Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?

Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe MWANGA WA JAMII

Wasiliana nasi

Simu: 0686 101335,

Barua pepe: advertise@guardian.co.tz



Wananchi na wafuasi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wakimkaribisha mgombea urais wa chama hicho, Dk. John Magufuli, alipowasili mjini Bukoba, mkoani Kagera juzi, tayari kwa mikutano yake ya kampeni za uchaguzi mkuu mkoani humo iliyoanza jana. **PICHA: IKULU**

# Magufuli aahidi kutatua kero sugu 12

**Na Gwamaka Alipipi,** BUKOBA

MGOMBEA urais kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, amewaahidi wananchi wa Mkoa wa Kagera kutatua kero sugu 12, zilizokuwa zinawasumbua kwa muda mrefu, mojawapo ni kukatika kwa umeme kila wakati.

Akiwa katika viwanja vya Gymkhana mkoani Kagera jana, Dk. Magufuli aliwahidi kuwatatulia kero hizo ambazo zimewatesa kwa muda mrefu, ndani ya miaka mitano ijayo, zingine hivi karibuni.

**UJENZI WA STENDI**

Akiwa katika viwanja hivyo, Dk. Magufuli aliwahakikishia wananchi na wa Manispaa ya Bukoba kuwajengea stendi ya kisasa, ambayo ujenzi wake umekwama tangu mwaka 2014 kutokana na mvutano wa wanasiasa.

"Ndugu zangu nileteeni mbunge Steven Byabato, kwenye kura za maoni alishika nafasi ya nne, lakini tulimchukua kwa sababu tulitaka kuvunja makundi Bukoba. Bukoba tumejichelewesha wenyewe, sasa nileteeni huyo ili stendi hiyo tuikamilishe," alisema Dk. Magufuli.

**SOKO KUBWA**

Dk. Magufuli alisema kumekuwa na tatizo la baadhi ya madiwani kulaumiwa kuuza vizimba vya kufanyia biashara, pamoja na wafanyabiashara wadogo kuuziwa kwa gharama kubwa.

Alitoa agizo kwa mamlaka husika kushughulikiwa kwa kero hiyo ndani ya muda mfupi kuanzia sasa.

**MGOGORO WA ARDHI**

Alisema kumekuwa na mgogoro wa ardhi eneo la Kiebitembe kwa muda mrefu kutokana na viongozi wa Manispaa ya Bukoba kuuza kiwanja kimoja kwa watu wengi.

"Namuagiza mkuu wa wilaya, maofisa ardhi waanze kushughulikia kero hii sasa hivi, hili zege haliwezi kulala".

**MTO KANONI**

Alisema kuwa Mto Kanoni umekuwa ukileta mafuriko ya mara kwa mara kwa wananchi mvua zinaponyesha. Aliagiza mamlaka husika kumaliza tatizo hilo ndani ya muda mfupi.

**MGOGORO WAFUGAJI, WAKULIMA**

Aliwahakikishia wananchi wa Wilaya ya Kyerwa kumaliza tatizo la mgogoro wa ardhi kati ya wakulima na wafugaji, ambao umedumu kwa muda mrefu.

**UJENZI BARABARA**

Vilevile, aliwaahidi wakazi wa Kagera kuwajengea barabara kutoka Umuru-Shaka-Karagwe hadi mpakani mwa Tanzania na Uganda (kilometa 90).

"Hili naomba mniachie mimi na mbunge wa Kyerwa tutalimaliza. Ni barabara inayounganisha Tanzania na Uganda."

**UJENZI WA MAHAKAMA, HOSPITALI**

Kadhalika, aliwaahidi wakazi wa Misenyi kuwajengea mahakama kutokana na wakazi wa eneo hilo kwenda umbali mrefu kupata huduma hiyo. Pia aliwaahidi kuwajengea hospitali ya wilaya.

**KUBORESHA MAWASILIANO**

Dk. Magufuli alisema katika eneo la Kanyigo, Mabare na sehemu zingine za makao makuu ya wilaya, wananchi wanakabiliwa na tatizo la mtandao wa mawasiliano ya simu.

Aliwahakikishia kumaliza kero hiyo ndani ya muda mfupi.

**MALIPO YA KAHAWA**

Alisema serikali itakwenda kulivalia njuga na kumaliza tatizo la ucheleweshaji wa malipo ya kahawa kwa wakulima.

"Haiwezekani wakulima wetu walipwe bei ya chini wakati nchi za jirani bei iko juu, ikiwezekana masoko ya nchi za jirani tutayaamishia hapa. Ninawahakikishia tutalipa madeni yote. Serikali ya CCM haiwezi kuwa ya kudhulumu, kama tulivyofanya kwenye pamba na korosho, ndivyo tutafanya kwenye kahawa."

**KERO YA MAJI**

Alisema katika kipindi cha miaka ijayo, serikali itamaliza tatizo la upatikanaji wa maji.

Katika kuhakikisha hilo, alisema serikali kwa sasa imeanza kutekeleza baadhi ya miradi ya maji na ifikapo Novemba, mwaka huu baadhi ya maeneo yatakuwa yameanza kupata maji.

"Tunataka maeneo ya mjini upatikanaji wa maji ufikie asilimia 87.6. kwa miaka mitano tumeshatekeleza miradi mingi yenye thamani ya Sh. bilioni 50.17."

**KUKATIKA KWA UMEME**

Alisema mkoa wa Kagera unakabiliwa na tatizo la kukatika kwa umeme kila wakati, pamoja na kutegemea kutoka nchi za jirani, hivyo serikali imeweka mikakati ya kuhakikisha tatizo hilo linapatiwa ufumbuzi, mojawapo ni kupata umeme kutoka katika maporomoko ya Mto Lusumo, Kakono yatakayokuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 87.

Pia mradi wa bwawa la Julius Nyerere litakalokuwa na uwezo wa kuzalisha umeme zaidi ya megawati 2,115 litasaidia kupatikana kwa umeme wa uhakika nchini.

Mbali na kutoa ahadi ya kutatua kero hizo, Dk. Magufuli alisema katika kipindi cha miaka mitano ijayo itahakikisha inavifufua viwanda vilivyokufa kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Alisema viwanda vya kilimo, nyama na maziwa, uvuvi, mazao mbalimbali vitapewa kipaumbelea katika kuviendeleza.

## Kabudi aponda Ripoti ya UN

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, ametoa kauli kuhusu ripoti ya Umoja wa Mataifa dhidi ya Tanzania inayoonyesha wasiwasi wa hali ya kisiasa, akisisitiza haina uhalisia.

Tume ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa ilitoa taarifa kuhusu haki za binadamu, kwenye maeneo mbalimbali duniani na kuonyesha wasiwasi wake kwa Tanzania.

Akijibu kuhusu ripoti hiyo jana katika mahojiano maalum na Shirika la Habari la BBC, Prof. Kabudi, alisema, wamepokea ripoti hiyo kwa mshangao mkubwa na wanaamini Kamishna wa Umoja wa Mataifa na Haki za Binadamu kwenye Tanzania, asingeandika au kutoa tathmini hiyo.

"Kwanza, tumechukua hatua ya kuhakikisha kwamba leo (jana), Balozi wa Tanzania Umoja wa Mataifa ofisi ya Geneva, anawasilisha majibu yetu rasmi kuhusu taarifa hii.

"Hali halisi ya Tanzania hailingani na hicho kilichotolewa, tunao wagombea wa urais 17 na wote wanafanya mikutano yao nchi nzima kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), mikutano hii inahudhuriwa na watu wengi."

Alisema, endapo hali ya kisiasa ingekuwa imeminywa isingekuwa jinsi ilivyo sasa, kampeni zimekuwa za amani na uchaguzi huo umetulia.

"Mgombea anasema anachotaka kusema na anayetukana, anatukana anavyoona na hakuna anayechukuliwa hatua kwa maana kwamba ni kipindi cha watu kusikia wagombea wakitoa hoja na hatimaye Oktoba 28, wachague marais, wabunge na madiwani Tanzania Bara na visiwani Zanzibar," alisema.

Hata hivyo, alisema siyo tabia wala ada ya Watanzania kupuuza kauli ya mtu yeyote, ni hulka yao kupokea mabaya na mazuri, ya kweli, uzushi, uongo, kashfa na sifa kwa sababu ya historia iliyopo.

"Ukisoma ripoti hiyo unaona kuna aina ya taswira ambayo inataka kuonyeshwa kwa dunia kwamba, serikali ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) chini ya uongozi wa Rais John Magufuli, imefanya maendeleo makubwa katika maeneo ambayo, mwaka 2015 yalikuwa yanapigiwa kelele," alisema.

Atoa mfano wa rushwa, ubadhirifu wa fedha za umma ambao ndani ya miaka mitano hakuna anayemnyooshea kidole, Rais Magufuli.

Prof. Kabudi alisema, Tanzania ilikuwa kitovu cha usafirishaji wa dawa za kulevya, uzembe katika utumishi wa umma, lakini kwa sasa hakuna anayemnyooshea kidole Rais.

Alisema, uchaguzi wa mwaka 2015 hayo ndiyo yalikuwa ajenda ya mataifa ya nje na vyama vya upinzani na ndani ya miaka minne yametatuliwa yote.

"Niwe mkweli, mara nyingi kiongozi wa Afrika akifanikiwa, wakishindwa kumkamata kwenye rushwa, ubadhirifu na kwenye mambo mengine lazima waanze kumwonyesha kwenye demokrasia na haki za binadamu," alisema.

Profesa Kabudi, alisema taswira hiyo hujengwa na mataifa mbalimbali siyo Umoja wa Mataifa.

"Ilani ya CCM sura ya sita inazungumzia haki za binadamu na maendeleo, nchi za Ulaya haki za kisiasa zinapewa umuhimu wa juu na nchi za Afrika zinapewa umuhimu ule ule, ambao pia zinapewa haki za kiuchumi na kijamii.

"Hakuna nchi duniani inayonyoosha kidole, ambayo bado haina changamoto za haki za binadamu, changamoto hizi zipo nchi zote hakuna wanaonyoosha vidole na sisi tunaonyooshewa vidole," alifafanua.

Alisisitiza kuwa Tanzania imechukua hatua zote kila siku kuzidi kuimarisha haki za binadamu.

Alitoa mfano kuwa, ndiyo nchi pekee ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, ambayo katika serikali za mitaa wameajiri mtu anayeshughulika kutoa msaada wa kisheria kwa watu wote wasiojiweza kwa makosa yote ya jinai na kesi za daawa.

"Hii ni hatua kubwa ya kulinda haki za binadamu, lakini yamkini kila mtu anafahamu kila nchi lazima iendelee kila siku kuhakikisha haki za binadamu katika nchi yake zinalindwa," alisema.

Kuhusu uhuru wa vyombo vya habari na kushikiliwa kwa wana harakati, Prof. Kabudi alisema kuwa, waandishi wa habari wengi nchini hawana mikataba ya ajira wala hifadhi ya jamii.

"Ukiangalia sheria ya vyombo vya habari imeangalia uhuru wa vyombo vya habari na maslahi ya waandishi wa habari, ili wapate ajira ya uhakika, mikataba, hifadhi ya jamii. Tumechukuwa hatua zote kuhakikisha vyombo vya habari vinafanya kazi."

Alisema, hakuna asasi au taasisi iliyofutwa au kufungwa, bali zinaangaliwa kwa lengo la kuhakikisha hazitumiki au kutumiwa vibaya.

Alifafanua kuwa waliozuiliwa fedha zao, ipo sheria ya uwazi na uwajibikaji na kwa sababu wanaishi katika kipindi kigumu cha ugaidi na utakatishaji fedha haramu, lazima serikali ijue zinatoka wapi na kwa ajili ya nini.

# Lema alia na kodi za utalii

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MGOMBEA ubunge Arusha Mjini kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Godbless Lema, amesema chama hicho kikipewa ridhaa ya kuongoza nchi, kitafuta utitiri wa kodi, ambao ni tatizo katika sekta ya utalii.

Akizungumza jana katika mkutano wake wa nane wa kampeni katika viwanja vya Soko la Kilombero jijini hapa, Lema alisema katika sekta ya utalii kuna zaidi ya kodi 36, ambazo ni kikwazo kikubwa kwa watalii, hivyo chama hicho kikishika dola kitafuta baadhi ya kodi zisizostahili kuwapo.

Akizungumza juzi katika moja ya mikutano ya kampeni jijini hapa, Lema alisema Tanzania ni moja ya nchi duniani zenye vivutio vingi vya utalii, lakini pato lake haliendani na vivutio vilivyopo.

"Tanzania ina vivutio vingi vya utalii, lakini pato la utalii na idadi ya watalii, haviendani na vivutio vilivyopo," alisema Lema huku akibainisha kuwa kwa mwaka Tanzania inapokea watalii milioni moja tu na idadi hiyo inachagizwa na wingi wa kodi kwenye sekta hiyo.

"Utalii Tanzania ni ghali kuliko nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki tunazopakana nazo, kwa mfano Kenya na Uganda na baadhi ya kodi zimekuwa moja ya sababu zinazofanya watalii kutokuja kutalii kwa wingi hapa kwetu," aliongeza. CHADEMA kama itashika dola, alisema watapeleka muswada bungeni wa kubadilisha baadhi ya sheria ambazo zimekuwa chanzo cha watalii kutokuja kwa wingi nchini na kupunguza mapato kwenye sekta ya utalii.

"Kazi ya Bunge ni kurekebisha sheria na sera, ili utalii uongezeke kutoka milioni moja hadi kufikia milioni 10 mpaka milioni 20 na kwa idadi ya vivutio tulivyo navyo inawezekana kabisa hakuna kitakachoshindikana kabisa," alisema Lema.

Akitoa mfano wa Malaysia, Lema alisema nchi hiyo ina vivutio vichache kulinganisha na Tanzania, lakini kwa mwaka inapokea watalii milioni 20 mpaka 30.

"Watalii wanaokuja kutalii kwenye nchi yetu ni wale wadogo ukilinganisha wale wanaokwenda kutalii kwenye mataifa mengine ndani na nje ya Bara la Afrika," alisema.

# Hussein Mwinyi 'aiteka' Pemba

**Na Rahma Suleiman,** PEMBA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), jana kilizindua rasmi kampeni zake kisiwani Pemba baada ya Septemba 12 kuzindua Unguja, mgombea wake wa urais, Dk. Hussein Mwinyi, akitamba kufanya kampeni wilaya kwa wilaya.

Akiwahutubia maelfu ya wananchi na wanachama wa CCM katika viwanja vya Gombani kisiwani hapa jana, Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, alisema mgombea wao huyo ni chaguo la CCM na chama hakikubahatisha kumsimamisha.

Dk. Shein alisema anaamini CCM Zanzibar itashinda kwa kishindo katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu na wananchi hawatofanya makosa wakikichagua tena chama hicho.

"Wembe ni uleule, wakitaka watanyolewa, wasipotaka watanyolewa," Dk. Shein alitamba.

Alisema mgombea wao, Dk. Mwinyi ana uwezo mkubwa wa kuiongoza Zanzibar, hivyo akaomba wananchi kumpigia kura katika uchaguzi huo.

Dk. Shein alisema kiongozi huyo ana uwezo mkubwa na ni mtu mwenye maadili na mchapakazi mahiri na anayejituma katika majukumu anayopewa kuyafanya. "Sisemi haya kwa kumtengenezea sifa, ninasema haya ndio aliyonayo mgombea wetu, ni mtu mwenye maadili, nidhamu na heshima yake haina shaka," alisema Dk. Shein.

Aliongeza kuwa Dk. Mwinyi ana sifa ambazo wagombea wengine wa vyama vya siasa hawana, akidai kuwa siyo mtu jeuri, hana kiburi wala hana tabia ya kuropoka ovyo. Akizungumza kwa niaba ya wagombea ubunge, uwakilishi na udiwani kisiwani Pemba, Profesa Makame Mbarawa Mnyaa, alisema Wazanzibari hasa Pemba, wanataka maendeleo na uchaguzi wa mwaka huu utakuwa wa kihistoria kwa CCM.

"Dalili ya mvua ni mawingu, Pemba mwaka huu tutaandika historia," alisema Mnyaa ambaye anawania ubunge mkoani kisiwani hapa.

Akinadi sera zake, Dk. Mwinyi alisema endapo akipata ridhaa za wananchi kuiongoza Zanzibar, atahakikisha maisha ya wananchi yanakuwa mazuri.

Alisema ataendeleza yote mazuri yaliyofanywa na serikali ya awamu ya saba ikiwamo elimu bure, afya bure na huduma nyingine muhimu kwa ajili ya maendeleo ya Zanzibar.

Alisema amedhamiria kufanya kazi kubwa ya maendeleo ya uchumi wa kisasa, akiahidi kuyafanya maisha ya wananchi kuwa bora kupitia uvuvi, utalii na viwanda.

Alisema kuwa Pemba kuna fursa nyingi na vivutio vingi, lakini idadi ya watalii wanaofika ni ndogo, hivyo atakuza sekta hiyo.

"Uchumi lazima uendane na uboreshaji wa huduma za jamii ikiwamo elimu, afya na huduma za majisafi na salama," aliahidi mgombea huyo.

Hata hivyo, Dk. Mwinyi alisema maendeleo hayatapatikana bila ya amani na utulivu, hivyo ni muhimu wananchi kuendelea kudumisha amani na utulivu uliopo nchini.

"Tusitoe nafasi suala la ubaguzi, lazima kupiga vita na kuwa wamoja," alisema na kusisitiza kuwa huwezi kuwa na uchumi wa kisasa kama hakutakuwa na utawala bora na kupinga vita rushwa, ubadhirifu wa mali, udhalilishaji na dawa za kulevya.

Uzinduzi huo ulipambwa kwa burudani ya muziki iliyotolewa na wasanii kutoka Zanzibar na Tanzania Bara.



Mgombea urais kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, akiwahutubia wananchi katika kampeni za uchaguzi mkuu Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Lissu kuruhusu mazao kuuzwa popote duniani

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MGOMBEA urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), amesema endapo atapata ridhaa ya wananchi kuongoza nchi, ataunda serikali, ambayo itaruhusu wakulima kuuza mazao yao mahali popote duniani. Aliyasema hayo jana, alipokuwa anahutubia maelfu ya wakazi wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi, mkoani Mbeya wakati wa uzinduzi wa kampeni za mgombea ubunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, kwa tiketi ya chama hicho, Joseph Mwasote 'China wa China'.

Lissu alisema, serikali yake itaweka utaratibu wa kuwawezesha wananchi kwenda kuuza mazao yao mahali popote watakapobaini kuwa kuna soko la uhakika la mazao yao, yakiwamo mataifa jirani.

Alisema atahakikisha anaifanya mikoa yote ya mipakani, ikiwamo ya Nyanda za Juu Kusini kuwa kanda maalumu za kiuchumi kwa kuruhusu mwingiliano wa kibiashara na mataifa jirani.

"Mtu akiwa na mahindi yake mengi ama mazao mengine anataka kwenda kuuza Zimbabwe, DRC (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo) na nchi nyingine yoyote, atawezeshwa na serikali, ili akauze apate hela aje afanye maendeleo," alisema Lissu.

Vile vile, alisema atahakikisha serikali yake inawafutia ushuru na tozo wafanyabiashara wadogo wakiwamo mamalishe na madereva bodaboda na bajaji, ili wafanye shughuli zao kwa uhuru, bila kubughudhiwa na maofisa wa serikali.

Alisema, akiingia madarakani atapeleka muswada wa sheria ndani ya siku 100, ambao utawezesha kufumuliwa kwa mfumo wa kodi uliopo na kuunda mpya, ambao utakuwa rafiki kwa wafanyabiashara na makundi yote yanayolipa kodi.

Alisisitiza kuwa, kila mlipa kodi atatakiwa kulipa kodi anayoimudu, badala ya mfumo wa sasa, ambao mfanyabiashara anakadiriwa na TRA na baadhi hukadiriwa kodi kubwa kuliko mapato yao halisi.

"Tutabadili katiba yetu iliyopo na kutengeneza mpya na tutaunda serikali, ambayo itakuwa rafiki kwa wananchi kwa kuwarejeshea madaraka, ili waamue aina ya maendeleo wanayoyataka," alisema na kuongeza.

"Sitakuwa dikteta kwa wananchi wangu, naombeni mniamini na muwaamini wagombea ubunge na udiwani wa CHADEMA, ili Oktoba 28 tuiongoze nchi hii," alisema Lissu.

Mgombea ubunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, Mwasote, alisema awali alienguliwa kushiriki kwenye kinyang'anyiro hicho na amerejeshwa hivi karibuni, baada ya Tume ya Uchaguzi (NEC), kuikubali rufani yake ya kupinga kuenguliwa.

Alisema, Jimbo la Mbeya Vijijini ni miongoni mwa majimbo ambayo yanakabiliwa na matatizo mengi, ikiwamo ubovu wa miundombinu ya barabara na hivyo akipata ridhaa ya wananchi, atahakikisha anapigania miundombinu hiyo iboreshwe.

Alisema wananchi wa wilaya hiyo ni wazalishaji wazuri wa mazao ya chakula na biashara, lakini barabara ni mbovu na zinawafanya washindwe kusafirisha mazao yao kwa urahisi, kwenda sokoni pamoja na kusafirisha pembejeo.

"Nawaombeni wananchi wa Mbeya Vijijini mnitume nikawatetee, ili miundombinu hii iboreshwe, kuna barabara hii ya Iwindi ni muhimu sana kwa kilimo na biashara, lakini ni mbovu na serikali ya CCM haitaki kuijenga," alisema Mwasote.

Tundu Lissu, anaendelea na harakati za kuomba kura kwa wananchi katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, kwa kuanzia mikoa ya Iringa na Njombe na baadaye Mbeya na Songwe.

# JPM aagiza mkuu wa shule iliyoungua aachiwe

**Na Gwamaka Alipipi,**
KAGERA

RAIS John Magufuli ameliagiza Jeshi la Polisi nchini kumwachia Mkuu wa Shule ya Msingi Byamungu Islamic, anayeshikiliwa baada ya kutokea kwa ajali ya moto na kuua wanafunzi 10, wengine sita kujeruhiwa.

Kadhalika, ameitaka Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kukagua na kuhakikisha shule zote na zinazoanzishwa zinazingatia masuala ya kisheria, lengo likiwa ni kuzuia matukio ya kuungua kwa shule kujirudia.

Alitoa agizo hilo jana mkoani Kagera wakati akizungumza na wananchi na wanachama wa CCM, waliojitokeza katika viwanja vya Gymkhana kumsikiliza.

"Wakati uchunguzi unaendelea juu ya tukio hilo la kuungua kwa shule, ninaomba mkuu wa shule aachiliwe, nikuombe RPC (Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa) umuachie...alianzisha shule kwa ajili ya watoto wetu kusoma na siyo kuwaunguza. Tukiendelea kumuweka ndani tunamwongezea mateso zaidi," alisema Rais Magufuli na kuongeza:

"Kama kuna uzembe ulifanyika basi hata akiwa nje upelelezi unaweza kufanyika na ataweza kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi. Nina imani huyu mkuu wa shule hana roho mbaya ya kuamua kuwachoma wanafunzi," alisema Rais Magufuli.

Shule ya Msingi Byamungu iliyoko kata ya Itera, wilayani Kyerwa iliteketea kwa moto juzi na kusababisha vifo vya wanafunzi hao.

Kadhalika, Magufuli ambaye anagombea urais kwa awamu ya pili, alielezea mafanikio yaliyopatikana katika Mkoa wa Kagera kwa kipindi cha miaka mitano.

Alisema Mkoa wa Kagera ulikuwa unakabiliwa na changamoto nyingi ikiwamo matukio ya ujambazi.

Alisema baadhi ya maeneo wananchi walikuwa wanashindwa kusafiri nyakati za usiku, ikiwamo msitu wa Kisindaga kwenda Karagwe, malori yalikuwa yanatekwa na majambazi.

"Leo hii matukio hayo yameisha na baadhi ya maeneo yamepungua, nivipongeze vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuhakikisha Kagera na Tanzania kwa ujumla inakuwa salama," alisema Rais Magufuli.

Aliongeza kuwa katika kuhakikisha Tanzania inakuwa salama, serikali iliamua kuyageuza baadhi ya mapori kuwa hifadhi za akiba, kama vile pori la Rumanyika, Burigi-Chato.

Kuhusu utalii, Rais Magufuli alisema serikali ina mkakati wa kuhakikisha ukanda wa Mkoa wa Kagera unakuwa wa utalii kama ulivyo wa Kaskazini.

Alisema: "Sekta ya utalii ndiyo inatengeneza ajira nyingi zaidi. Kwa kipindi cha miaka mitano imetengeneza ajira milioni nne. Mwaka 2019 ilichangia Sh. bilioni 2.6 ikishika nafasi ya pili baada ya sekta ya madini kuongoza kwa kuingiza Dola za Marekani bilioni 2.7."

Kuhusu elimu, alisema serikali katika kipindi cha miaka mitano imejenga shule za msingi 27 mkoani Kagera, shule za sekondari 28, pamoja na kutoa Sh. bilioni 57.23 kufanikisha elimu bure.

Alisema pia walimu 1,658 wameajiriwa mkoani humo kwa kipindi cha miaka mitano, ujenzi wa madarasa 1,119 pamoja na ujenzi wa nyumba za walimu 286.

Aliahidi atakapostaafu atahamishia makazi yake mkoani Kagera.

**KAULI YA MUFTI**

Akizungumzia tukio hilo jana jijini Dar es Salaam, Mufti Mkuu wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zuberi, aliagiza wamiliki wa shule nchini waimarishe ulinzi ndani ya shule zao na kuchukua tahadhari za kina na kuhakikisha mifumo ya umeme, uzio na vifaa vya kuzima moto vinakuwapo.

Alisema Baraza Kuu la Waislam linaendelea kusubiri taarifa rasmi ya vyombo vya ulinzi na usalama.

"Baada ya taarifa hii ya moto nilituma ujumbe wa viongozi wa Bakwata Mkoa wa Kagera ukiongozwa na Katibu Mkoa na wenzake ambao walituthibitishia ajali hii ya moto.

"Ninatoa pole kwa mkuu wa shule na wazazi waliopoteza watoto na waliojeruhiwa katika ajali hii, pole kwa Rais Magufuli, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mkuu wa Mkoa wa Kagera na Sheikh wa Mkoa huo na mmiliki wa shule," alisema.

**●Imeandaliwa na Romana Mallya, Frank Maxmillian (DAR), Gwamaka Alipipi na Lilian Lugakingira (BUKOBA)**



Mufti wa Tanzania Sheikh Abubakar Zuberi, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu tukio la ajali ya moto katika Shule ya Msingi Byamungu Islamic, mkoani Kagera. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kamanda Shana afariki dunia

**Na Enock Charles**

ALIYEKUWA Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Jonathan Shana, amefariki dunia usiku katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), alikokuwa anapatiwa matibabu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano hospitalini huko, Aminiel Aligaesha, Shana alifariki dunia usiku wa kuamkia jana.

Aligaesha alisema kuwa kabla ya kupatwa na umauti, Shana alikaa hospitalini huko kwa siku 21 na kati ya hizo alikaa katika chumba cha uangalizi maalum (ICU) kwa siku tatu.

"Jonathan Shana, RPC (Kamanda wa Polisi Mkoa) Mkoa wa Arusha amefariki usiku wa kuamkia leo Septemba 16, 2020, amelazwa hapa Muhimbili kwa siku 21, na kati ya siku hizo ICU amekaa siku 3", alisema Aligaesha.

Ikumbukwe kuwa Juni 24, mwaka huu, Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Simon Sirro, alimhamisha Shana kutoka kuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha kwenda kuwa Ofisa Mnadhimu Shule ya Polisi Moshi.

Akizungumzia msiba huo, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, alisema: "Nimepokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kifo cha Kamanda Shana. Wiki iliyopita, nilikwenda kumwona Muhimbili ambako alilazwa karibuni wiki tatu na nilipta matumaini makubwa. Jamani Kamanda Shana! Bwana ametoa na ametwaa... Jina la Bwana libarikiwe!"

Gambo kwa sasa anawania ubunge wa Arusha Mjini kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), akichuana na Godbless Lema (CHADEMA) ambaye amejitosa tena kutetea kiti chake.

# Uhamiaji kupitia mapingamizi uraia

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

IDARA ya Uhamiaji imeahidi baada ya uchaguzi mkuu kufanyika itaharakisha mchakato wa kupitia mapingamizi ya shaka ya uraia wa baadhi ya wananchi mkoani hapa, ili wanaostahili wapate vitambulisho vya taifa.

Hayo yamebainishwa na Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dk. Anna Makakala, alipokuwa kwenye ziara yake ya kikazi mkoani hapa kuwa amebaini mkoa huo kuwa na changamoto kubwa ya mchakato wa Vitambulisho vya Taifa na kuwa kero kwa wananchi.

Alisema walijipanga kuharakisha mchakato huo, lakini mlipuko wa ugonjwa wa virusi vya corona nchini ulisababisha kusimama hivyo wananchi waendelee kuwa na matumaini.

Makakala alisema kwa sasa wanawaacha wananchi waendelee na mchakato wa uchaguzi, ili wapate fursa ya kusikiliza sera mbalimbali kutoka kwa vyama vya siasa kwa kuwa ni haki yao na baadaye ndipo mchakato wa kupitia mapingamizi na uhakiki wao utafanyika kwa haraka.

"Nimebaini Mkoa wa Kigoma una changamoto kubwa ya upatikanaji wa Vitambulisho vya Taifa, wananchi waendelee kuwa wavumilivu, baada ya uchaguzi jambo hili litafanyiwa kazi kwa haraka," alisema.

Mwananchi mkoani hapa, Godbert Ichila, alisema kukosekana kwa namba za utambulisho wa taifa ni kikwazo kwao katika utendaji kazi wa kila siku kwa kuwa baadhi yao bado hawana mawasiliano ya simu kutokana na laini zao kufungiwa huku pia akieleza kupata changamoto katika masuala ya upokeaji fedha kwa njia ya mitandao ya simu.

"Kwa dunia ya leo kukosa simu ni kama kuwa gizani tunawaomba wahusika watambue kero hii kuwa ni kubwa na wachukue hatua," alisema.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Kamishna wa Polisi, Thobias Andengenye, alisema changamoto hivyo ni kubwa na ya muda mrefu, lakini bado umakini mkubwa unahitajika kufanikisha jambo hilo.

Alisema wamekuwa wakiwasihi wananchi kuwa wavumilivu kwa kuwa mkoa huo umepakana na nchi jirani ya Burundi ambayo kuna mwingiliano mkubwa hivyo serikali isipokuwa makini raia wa nchi jirani wanaweza kujipenyeza katika mchakato huo.

# Watano wafa ajali ya basi, 6 wajeruhiwa

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

WATU watano wamefariki dunia na wengine sita kujeruhiwa baada ya basi la abiria aina ya TATA kuacha njia na kuligonga gari aina ya Isuzu.

Ajali hiyo ilitokea jana majirà ya mchana katika Kijiji cha Msanga Kata ya Mitesa mpakani mwa wilaya za Masasi na Newala, mkoani Mtwara.

Majeruhi hao sita na miili ya watu waliofariki walipelekwa katika Hospitali ya Wilaya ya Newala.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Mark Njera, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo na kuwatakà madereva wa vyombo vya moto kuwa waangalifu barabarani kwa kuzingatia sheria za usalama barabarani.

Kamanda Njera alisema basi hilo la abiria lilikuwa likitokea wilayani Masasi kuelekea wilayani Newala hadi Tandahimba.

Alisema lilipofika maeneo ya Kijiji cha Msanga Kata ya Msanga ndipo lilipokutana na Isuzu yenye namba za usajili T-311 AER, ambalo lilikuwa likitokea wilayani Newala kuelekea Kijiji cha Mchauru kata ya Mchauru wilayani Masasi mkoani Mtwara.

Kamanda Njera alisema magari hayo yaligongana uso kwa uso, hivyo kusababisha vifo hivyo na majeruhi.

Alisema majeruhi walikimbizwa katika Hospitali ya Wilaya Newala.

"Tunaendelea kuwasihi madereva wa vyombo vya moto kuzingatia sheria zote za usalama barabarani, ili kunusuru maisha ya watu wasio na hatia kama kila dereva akifuata sheria kikamilifu ajali zitapungua," alisema Kamanda Njera.

Alisema wananchi wanatakiwa kwenda Hospitali ya Wilaya ya Newala kwa ajili ya kutambua miili ya waliokufa.




Askari wa kikosi cha usalama barabarani akikagua basi aina ya Tata la kampuni ya White Star Express, lililokuwa likitokea wilayani Masasi kwenda Newala-Tandahimba kugongana uso kwa uso na basi aina ya Isuzu Journey lenye namba za usajili T 331 AER katika kijiji cha Msanga, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, mkoani Pwani jana .**PICHA: HAMISI NASRI**

# Matiko awaomba Tarime wamrejeshe bungeni

**Na Timothy Itembe,** TARIME

MGOMBEA ubunge Jimbo la Tarime Mjini mkoani Mara, kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Esther Matiko, ameomba wananchi wa jimbo, kumwamini na kumchagua kwa kura nyingi zitakazompa ridhaa ya kwenda bungeni, ili kuwawakilisha kwa mara nyingine.

Matiko alibainisha hayo jana, kwenye mkutano wa kampeni uliofanyika viwanja vya Mtaa wa Sabasaba mjini hapo, ambapo alisema kuwa wananchi wa Tarime hana wasiwasi nao kwa kuwa watamchagua kuwa mwakilishi wao kwa mara nyingine, kwa sababu ameshirikiana nao vizuri kipindi kilichopita akiwa mbunge.

"Wananchi wangu nawapenda, najua hamtaniangusha mtanipa kura za kutosha kwa sababu nimeshirikiana nanyi vyema katika shughuli za maendeleo kama kuchimba visima vinne, mradi wa maji wa shilingi bilioni moja, ambao ukianza mitaa yote 81 ya Tarime Mjini itanufaika ikiwamo miradi ya elimu na afya," alisema Matiko. Matiko aliongeza kuwa mafanikio hayo hayakuja bure, bali walishirikiana na Halmashauri ya Mji wa Tarime, kupitia madiwani wakiongozwa na mwenyekiti wake, Hamis Nyanswi.

Mgombea huyo, alitumia nafasi hiyo kulaani baadhi ya watu wanaotoa kauli za udhalilishaji wa wanawake, kwa kudai kuwa Halmashauri ya Tarime Mjini haiwezi kuongozwa na mwanamke, licha ya kuwa hata Rais John Magufuli alishawahi kusema kuwa wanawake wakipewa nafasi wanaweza.

Matiko aliwataka wananchi wa Mtaa wa Sabasaba kuwa watulivu wakati Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ikiendelea kusikiliza rufani ya wagombea wao ambao, waliwekewa mapingamizi akiwamo, Pamba Chacha, mgombea udiwani kupitia CHADEMA na Bashiri Selemani na kuwa wasiwe na wasiwasi rufani yao itarudi na watakuwa wagombea.

# Chikota ataja vipaumbele 5 Nanyamba

**Na Mwandishi Wetu,** MTWARA

MGOMBEA ubunge wa Jimbo la Nanyamba mkoani Mtwara kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Abdallah Chikota, amezindua kampeni zake huku akitaja mambo muhimu matano atakayoyafanya endapo atachaguliwa.

Akizungumza jana kwenye uzinduzi wa kampeni za CCM, uliofanyika kwenye Kata ya Mtiniko, Chikota alitaja mambo hayo kuwa ni kuboresha sekta ya afya kwa kuongeza vituo vya afya, zahanati kwenye maeneo ambayo hayana na kukamilisha ujenzi wa majengo yaliyobaki kwenye ujenzi wa hospitali ya wilaya.

Kuhusu sekta ya maji, mgombea huyo alisema atahakikisha anasimamia ukamilishaji wa mradi wa maji ulioanza Nanyamba na Chawi.

"Nitahakikisha nafuatilia serikalini kuhusu uanzishaji wa mradi wa maji mkubwa, ili kusaidia kata tano ambazo zina shida kubwa ya maji zikiwamo Mnima, Nyundo, Timbwilimbwi, Njengwa na Nitekela," alisema.

Akizungumzia sekta ya elimu, aliahidi kuendelea kuboresha sekta ya elimu kwa kuboresha miundombinu ya shule kwa kujenga madarasa, nyumba za walimu na matundu ya vyoo.

Kadhalika, alisema atahakikisha anasimamia serikali kukamilisha vijiji 52 ambavyo vimebaki bado havijapata umeme.

"Naomba mnichague tena kwa kipindi kingine cha miaka mitano, pia mchague Rais John Magufuli na wagombea wote wa CCM na madiwani wa kata zote 17 ili kuharakisha maendeleo ya Nanyamba.

"Katika miaka mitano iliyopita, mmeshuhudia mafanikio mengi kwenye sekta mbalimbali, miaka mitano ijayo pia nitasimamia serikali kuongeza fedha zinazotengwa kwa ajili ya TARURA kukamilisha miradi ya barabara vijijini na kuweka lami kwenye vilima korofi," alisema.

Katika mkutano huo, mgombea huyo alitaja mafanikio mbalimbali yaliyopatikana kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita kuwa ni ujenzi wa hospitali ya wilaya iliyogharimu zaidi ya Sh. bilioni moja, ujenzi wa vituo vya afya vitatu vya Majengo, Dinyecha na Kilomba vilivyogharimu Sh. bilioni 1.4.

"Kuna ujenzi wa zahanati 11 unaendelea, lakini halmashauri imepata magari matatu ikiwamo gari moja la mganga mkuu na mengine ya wagojwa (ambulance)," alisema.

Pia alisema wananchi wamenufaika na ujenzi wa barabara ya Mtwara-Mnivata kwa kiwango cha lami unaoendelea na barabara za mzunguko za ndani katika halmashauri ambapo kila mwaka zinajengwa kilometa mbili kwa kiwango cha lami hivyo kufikia kilometa 11 .8 huku Shirika la Mawasiliano ya Simu Tanzania (TTCL) likijenga minara 11 ya simu.

"Kwa hiyo ndugu zangu mnaona dhahiri mafanikio na faida inayofanywa na CCM tusifanye makosa mara mbili, tufanye maamuzi sahihi tuchague Chama Cha Mapinduzi ili tuzidi kunufaika na maendeleo katika halmashauri yetu na mkoa kwa ujumla," alisema Chikota.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uhamiaji izitatue kero hizi mipakani

**BAADHI** ya kero zinazotokea katika maeneo ambayo nchi yetu inapakana na mataifa jirani, zinaweza kutatuliwa kama mamlaka za serikali zitawajibika ipasavyo kwa kuzifuatilia kwa karibu na kuchukua hatua.

Ikumbukwe kwamba Tanzania ina eneo kubwa, na ni miongoni mwa nchi kubwa kwa eneo barani Afrika, hivyo kupakana na nchi za Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia (DRC), Malawi, Zambia na Msumbiji.

Kutokana na hali hiyo, ni dhahiri kuwa matatizo na kero haviwezi kuepukika katika maeneo yote ya mipaka kati ya Tanzania na nchi hizo.

Maeneo ambayo yamekuwa yakikabiliwa na changamoto zinazotokana na masuala ya uraia ni katika mikoa inayopakana na nchi zenye matatizo kadhaa hasa migogoro ya kisiasa.

Kutokana na hali hiyo, nchi yetu imekuwa ikijikuta inaathirika kutokana na ujio wa wakimbizi na raia wengine wa nchi jirani ambao si wakimbizi rasmi kwa mujibu wa sheria na taratibu za Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Wakimbizi (UNHCR), bali kuja kuishi katika mazingira yenye uhakika wa usalama.

Kutokana na mazingira ya amani na utulivu ulioko nchini tangu wakati wa Uhuru mwaka 1961, raia wa nchi jirani wamekuwa wakimiminika nchini na kunusuru maisha yao kutokana na machafuko kwenye nchi zao.

Jambo la kupongeza ni kuwa nchi yetu na raia wake wamekuwa wakarimu na wavumilivu kutokana na kutochoka kuwapokea wageni na kuwapa hifadhi, huku wakizivumilia changamoto ambazo zimekuwa zikisababishwa na ujio wao yakiwamo matukio ya uhalifu na uharibifu wa mazingira.

Pamoja na hali hiyo, kuna baadhi ya matatizo yanaendelea kujitokeza hususan wahamiaji haramu wanaoingia nchini katika maeneo ya mipakani na kuajiriwa kufanyakazi.

Akiwa mkoani Kigoma mapema wiki hii, Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dk. Anna Makakala, aliwaonya baadhi ya wananchi wa Mkoa huo wanaohifadhi raia kutoka Burundi na kuwatumikisha mashambani pasipo kufuata taratibu za kisheria.

Makakala alitoa onyo hilo wakati wa ziara yake ya kikazi mkoani humo ya kukagua maeneo yanayopakana na Burundi katika wilaya za Kibondo na Kakonko kwenye mipaka ya Muhange na Mkalazi. Alisema wananchi wanatakiwa kuhakikisha suala la ulinzi na usalama linahimarika katika mikoa hii iliyoko mipakani, na kuwa dara ya Uhamiaji itaendelea kusimamia.

Dk. Makakala alisema endapo taratibu rasmi zitatumika kuwaingiza raia hao nchini, itasaidia kuwafuatilia kama wamerejea nchini kwao baada ya msimu wa kilimo kupita na kama sivyo hatua za kuwafuatilia walikoelekea kufanyika.

Mkuu wa Wilaya ya Kakonko, Kanali Hosea Ndagala, alisema wilaya hiyo ina mipaka mikubwa ya wazi yenye zaidi ya kilomita 40, hivyo kuiomba Uhamiaji kuongeza nguvu kazi zaidi katika wilaya hiyo itakayowezesha kusimamia vyema.

Pia alisema wilaya hiyo ni mapito ya raia wa Burundi wanapokuwa wanakwenda katika maeneo mengine nchini, hivyo, kazi ya kuwabaini inakuwa ngumu.


Mmoja wa raia wa Burundi, alisema wanalazimika kutembea umbali mrefu kutoka mpaka wa Muhange hadi Kakonko kufuata vibali vya kuingia nchini kutokana na eneo la mpaka huo kutokutoa huduma hiyo, hivyo kuomba usogezwaji wa huduma karibu.

Changamoto zilizobainishwa kwa Kamishna Jenerali Makalala ni sehemu ya zinazotokea katika maeneo mengine ya mipakani, hivyo tuna uhakika amezisikia na kilichobaki sasa ni kwa Idara ya Uhamiaji kuzitafutia ufumbuzi ili zisijirudie.

Ushauri wetu ni kwamba Uhamiaji iangalie uwezekano wa kupanua wigo katika ufuatiliaji wa vibali vya raia wanaotoka nje hususan wa Burundi ili kuwawezesha kuingia nchini wakiwa na vibali halali. Tumeitaja Burundi kwa kuwa ndiyo nchi jirani ambayo imekuwa ikikumbwa na mizozo mara kwa mara, na kuwalazimisha raia wake kukimbilia nchini kana wakimbizi halali na wengine kuingia kutafuta maisha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Juhudi zahitajika kuilinda biyoanuai

Na Gaudensia Mngumi

**UMOJA** wa Mataifa (UN) unaeleza kuwa, upotevu wa biyoanuai (viumbe hai wanyama na mimea) umefikia rekodi ya viwango vya juu na vya kutisha.

Inataja mfano kuwa hekta bilioni mbili za ardhi zimepoteza rutuba, lakini aina zaidi ya 1,000,000 za wanyama na mimea inayopatikana sehemu mbalimbali duniani ziko katika hatari ya kutoweka.

Watu wanazidi kuwa hatarini zaidi kwa vitisho vipya vya magonjwa kama janga la virusi vya COVID -19 na maradhi yanayoambukizwa virusi.

Hayo ni kwa mujibu wa ripoti kuhusu bayoanuai ya dunia, iliyotolewa Jumanne wiki hii na UN

Ripoti hiyo inayotathmini mafanikio ya utekelezaji wa Mpango Mkakati ya Ulinzi wa Bayoanuwai katika mwaka 2011 hadi 2020, ikiwa imeandaliwa na wataalamu kutoka kongamano la utofauti wa bayoanuai.

Wanaeleza kuwa kati ya malengo 20 yaliyowekwa, ni sita tu kati ya hayo ambayo yamefikiwa. Lakini hata hivyo imeonekana kuwa si matokeo mabaya, wakionyesha kuwa juhudi za pamoja kulinda bayoanuai zinasaidia kuokoa viumbe vyote.

"Kwa hivyo, katika miongo mitatu iliyopita, takribani aina 50 za ndege na wanyama ambao walikuwa hatarini kupotea. Wameokolewa au kuhifadhiwa na 25 miongoni mwazo, katika muongo mmoja wa mwisho."

Wataalamu wanaeleza pia karibu theluthi ya mashamba yote duniani sawa na mashamba milioni 163 yanatumia njia endelevu za kilimo. Kiwango cha ukataji misitu kimepungua kwa asilimia 33. Hekta 22 za ardhi hivi sasa ziko katika kurejeshwa katika hali yake.

**Wataalamu wanaeleza pia karibu theluthi ya mashamba yote duniani sawa na mashamba milioni 163 yanatumia njia endelevu za kilimo. Kiwango cha ukataji misitu kimepungua kwa asilimia 33. Hekta 22 za ardhi hivi sasa ziko katika kurejeshwa katika hali yake.**

Wataalamu wanasisitiza kuwa takwimu zote hizo zinaonyesha kuwa hali ni ya kutia matumaini na jumuiya ya kimataifa inatakiwa kuongeza juhudi maradufu ili kuhifadhi na kuilinda bioanwai. Wataalamu hao wanaainisha maeneo manane ya vipaumbele kwa ajili ya kuchukua hatua zaidi katika eneo hili la utunzaji biyoanuai.

Kulinda, ardhi na misitu ni jambo la kwanza na nia ni kudhibiti mmomonyoko wa udongo na kurejesha mfumo wa asili wa misitu.

Pili wataalamu wanasema mabadiliko katika njia za kilimo kwa kutumia njia bora zinazofuata mifumo ya asili ili kuboresha tija na kupunguza athari mbaya kwenye bayoanuai.

Tatu wanapendekeza kufanya mabadiliko ya ulaji ikiwamo kuhamasisha maisha ya kula kunakozingatia afya na umuhimu wa kutumia vyakula vya mimea zaidi kuliko wanyama.

Eneo la nne ni kurejesha mzunguko wa ikolojia halisi ya baharini na kuendeleza ufugaji wa samaki.

Jambo la tano ni kuhakikisha matumizi ya njia endelevu katika ujenzi wa miji na utengenezaji wa miundombinu rafiki kwa mazingira.

Jambo jingine ni kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, ikiwamo kutokomeza nishati yatokanayo na mabaki ya wanyama. Aidha , kuanzishwa kwa kanuni ya mwingiliano wa usawa wa mifumo yote ya ikolojia zinazodhibiti uharibifu wa maisha ya bayoanuai.

Watalaam hao wanasisitiza umuhimu wa kutenga bajeti za kutosha kwa ajili ya shughuli za utunzaji wa bayoanuai na kwamba dola bilioni 100 zinatengwa kila mwaka kwa ajili ya suala hili, ingawa mabilioni ya dola nyingine yanahitajika, inaeleza ripoti hiyo.

HABARI PICHANI

# HEKA HEKA ZA KAMPENI ZA UCHAGUZI MKUU



Mgombea ubunge wa Jimbo la Monduli kupitia tiketi ya CCM, Fredrick Lowassa, akisalimiana na makada wa chama hicho, kabla ya kuhutubia mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu katika Kata ya Olosokwani, wilayani Monduli, Mkoa wa Arusha jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) wa Wilaya Arusha Mjini, Ephata Nanyaro, akiwaombea kura wagombea urais, ubunge na udiwani wa chama hicho, katika mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu jijini Arusha juzi. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**



Mgombea ubunge wa Jimbo la Arusha Mjini kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mrisho Gambo, akiwa amebebwa juu na wanachama na mashabiki wa chama hicho, kabla ya kuhutubia mkutano wa ufunguzi wa kampeni za uchaguzi mkuu jijini Arusha juzi. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**



Mgombea mwenza wa kiti cha urais kupitia Chama cha Sauti ya Umma (SAU), Satia Mussa Bebwa, akijinadi kwenye mkutano wa kampeni za chama hicho, eneo la Segerea, jijini Dar es Salaam, juzi, huku mgombea urais, Muttamwega Mgaywa akiwa juu ya gari. **PICHA: SABATO KASIKA**



Wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na wananchi wa Jimbo la Peramiho wakimsikiliza mgombea mwenza wa urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa tiketi ya CCM, Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan, alipokuwa akiwahutubia kwenye mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu katika uwanja wa Tamasha Peramiho (A) Wilaya ya Songea Vijijini, mkoani Ruvuma jana. **PICHA: OMR**



Mgombea udiwani Kata ya Ngokolo, Manispaa ya Shinyanga kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Emmanuel Ntobi, akinadi sera zake kwa wananchi katika mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu, uliofanyika katika kata hiyo, juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**




Aliyekuwa Mbunge wa Chumbuni, Ussi Salum Pondeza (wa pili kulia) akitumia simu yake kuingia kwenye mfumo wa Benki ya CRDB wa kupokea maoni kwa njia ya Kidigitali QR Code, katika hafla ya uzinduzi wa mfumo huo, katika tawi la Benki hiyo, Kisiwandui, mjini Unguja juzi. Wangine (kutoka kushoto) ni Maneja Huduma kwa wateja, Queen Odunga, Meneja wa Kanda wa Benki ya CRDB, Badru Idd na Meneja wa Tawi hilo, Mbwana Ahmed. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watoa huduma malazi watolewa hofu usajili wa wageni kidijitali

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii, imewatoa hofu wamiliki wa huduma za malazi katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara kuhusu usajili wa wageni kwenye mfumo wa MNRT Portal.

Mfumo huo utakaoanza kutumika nchini kote Oktoba Mosi, kwa mujibu wa serikali umelenga kupata takwimu sahihi za wageni zitakazosaidia kuboresha sekta ya utalii nchini na si vinginevyo.

Pia mfumo huo utalinda siri za wageni na zitatumika kwa ajili ya matumizi ya serikali pekee. Kaimu Mkurugenzi wa Utalii, Philip Chitaunga, alisema hayo jana jijini Arusha alipokuwa akihitimisha mafunzo yaliyofanyika kwa siku mbili kwa ajili ya usajili wa wageni kwenye mfumo wa MNRT Portal kwa zaidi ya watoa huduma za malazi 250 wa mikoa hiyo. Alisema usajili wa wageni katika mfumo huo utahusisha wageni wa ndani na wa nje ya nchi na lengo kuu ni kupata takwimu zitakazosaidia kuboresha sera, mikakati na mbinu za kukuza utalii nchini.

Chitaunga alisema usajili huo, mbali ya kusaidia kujua idadi ya watalii wa ndani, utawasaidia hata wamiliki wa malazi hayo kuweka rekodi za wageni waliolala katika malazi yao kwa kipindi chote ambacho wanafanya biashara hiyo ya malazi.

Katika sekta ya utalii, alisema mfumo huo umekuwa ukitumika sehemu nyingi duniani kama vile Uingereza, Marekani na Canada, hivyo si kitu kipya kilichoanzishwa nchini.

Pia alisema mfumo huo utasaidia kurahisisha kazi kwa wamiliki wa malazi, ambapo badala ya kubeba karatasi na kwenda katika ofisi za Wizara ya Maliasili na Utalii kwa ajili ya kulipia leseni, watatumia kompyuta tena wakiwa ofisini kwao kufanya usajili huo.

Mkurugenzi huyo alisema mfumo huo utakaoanza kutumiwa na watoa huduma za malazi nchini kote Oktoba Mosi, mwaka huu, utahusisha hoteli kubwa, za kati (lodge), nyumba za wageni na mahema ya watalii.

Alitaja vitambulisho vitakavyotumika katika usajili huo kuwa ni kitambulisho cha Taifa kwa wageni ambao ni Watanzania na pasi ya kusafiria kwa wageni wa kutoka nchi za nje. Chitaunga pia alisema kuanza kutumika kwa mfumo huo ni utekelezaji wa takwa la kisheria linalomtaka kila mmiliki wa malazi kuanza kusajili wageni kwenye mfumo wa MNRT Portal.

Pia alisema matumizi ya mfumo huo utaifanya sekta ya utalii kwenda katika uchumi wa bluu utakaoiweka Tanzania katika mazingira bora ya kibiashara.

Naye Anne Sostheness, mmoja wa wamiliki wa malazi katika mkoa wa Arusha aliyeshiriki mafunzo hayo, alisema mafunzo ni mazuri na ni salama kwa mteja na mtoa huduma kwa sababu mteja anatakiwa kuonyesha kitam-

# TMDA yazima ndoto wakaguzi feki

**Na Anthony Gervas,**
MWANZA

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), imezindua vitambulisho vipya vya ukaguzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi ili kuwadhibiti matapeli waliokuwa wakighushi vitambulisho vya awali wakijifanya maofisa wakaguzi wa taasisi hiyo.

Uzinduzi huo ulifanyika jana jijini Mwanza katika ofisi za mamlaka hiyo, ambao ulihudhuliwa na wajumbe wa bodi ya ushauri, wakaguzi toka halmashauri mbalimbali, wafamasia na wakaguzi wa mamlaka hiyo. Akizindua vitambulisho hivyo, Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Prof. Mabula Mchembe, aliwataka watumishi wa mamlaka nchini kuvitumia vizuri kama ilivyokusudiwa katika kazi zake.

"Tunavitaka vyombo vya ulinzi na usalama nchini likiwamo Jeshi la Polisi, kushirikiana na halmashauri kufuatilia na kuwabaini watu watakaovighushi vitambulisho vipya ili kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu," alisema.

Prof. Mchembe alisema sera ya afya iliyoandaliwa na wizara, imeweka kipaumbele kuhakikisha dawa, vifaa tiba na vitendanishi vitakavyotumika nchini ni vile vilivyothibitishwa ubora, usalama na ufanisi wake ili kumlinda mtumiaji.

Alisema mamlaka za udhibiti, kama ilivyo TMDA duniani kote, zina wajibu wa kulinda afya ya jamii na uhakika wa kupata bidhaa bora na salama kwa matumizi ya binadamu na zinazotibu.

Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Adam Fimbo, alibainisha kuwa vitambulisho 524 vimeandaliwa, kati ya hivyo, 387 ni kwa ajili ya wakaguzi wa halmashauri, 137 kwa ajili ya wakaguzi walioko TMDA, ambavyo vimelenga kuzifikia halmashauri 143.

Fimbo alisema mamlaka imeweka mifumo mbalimbali ikiwamo usajili wa bidhaa husika, usajili wa maeneo ya biashara ya bidhaa na uchunguzi wa kimaabara wa bidhaa husika ili kuhakikisha ubora na usalama wake, ukaguzi wa maeneo yote yanayohusika na utengenezaji, usambazaji na uuzaji wa bidhaa hizo.

Mifumo mingine ni pamoja na udhibiti wa mipaka na uingizaji nchini au utoaji nje ya nchi wa bidhaa, ufuatiliaji wa usalama wa dawa kwenye soko, uchukuaji sampuli na upimaji wa ubora wa bidhaa, uondoaji kwenye soko na uteketezaji wa bidhaa zisizofaa kwa matumizi ya binadamu pamoja na utoaji wa elimu kwa umma, ili kuelimisha jamii juu ya matumizi sahihi ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi

# NEMC yajivunia miaka mitano ya JPM

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limesema limepata mafanikio katika kutekeleza majukumu yake, katika kipindi cha miaka mitano ya uongozi wa Rais Dk. John Magufuli.

Hayo, yalibainishwa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, na kufafanua kuwa katika miaka mitano iliyopita NEMC imeweza kujipambanua kama taasisi muhimu, katika kufanikisha azma ya serikali ya ujenzi wa viwanda na kuimarisha msingi wa uchumi wa kati.

"Katika kipindi cha miaka mitano serikali ya Dk. John Pombe Magufuli NEMC, imekewa mazingira rafiki na kuondoa baadhi ya vikwazo, ambavyo vilifanya NEMC kushindwa kusimamia utekelezaji wa majukumu yake," alisema Dk. Gwamaka na kutaja sehemu ya mafanikio hayo ni kuzuia matumizi ya mifuko ya plastiki. NEMC pia huratibu na kutoa ushauri juu ya kulinda maeneo makubwa kama hifadhi za taifa na namna nzuri ya kupambana na athari za mabadiliko ya tabia ya nchi.

Dk. Gwamaka alisema, NEMC imejenga utaratibu wa kukutana na wawekezaji na wafanyabiashara na kwamba, kwa pamoja wamekubaliana juu ya umuhimu na faida ya kutunza mazingira, kwa manufaa ya ustawi wa jamii ya Watanzania na dunia kwa ujumla.

"Katika kipindi cha miaka mitano tumekutana na wawekezaji pamoja na wafanyabiashara, ili kujadiliana mambo muhimu ya mazingira, ambayo yalionekana kuwa ni changamoto kubwa na kuyapatia ufumbuzi na pia, waliweza kutambua NEMC kama chombo wezeshi na kinachosimamia watu wafuate sheria na taratibu za mazingira," alisema na kuongeza kuwa, NEMC imepunguza siku za utoaji vibali vya Athari ya Tathmini kwa Mazingira (TAM).

Alisema katika kipindi hicho NEMC imeweza kushirikiana na vyombo vingine, kuhakikisha malengo ya serikali yanatimia kwa kuondoa vikwazo visivyo na lazima na kuongeza kwamba, NEMC imewahimiza wawekezaji na wafanyabiashara kutunza na kulinda mazingira kwa manufaa ya vizazi vya leo na vijavyo.

"Mbali ya kutoa elimu kwa wawekezaji na wafanyabiashara, baraza limeondoa vikwazo kadhaa ambavyo vilikuwa vinachelewesha mchakato wa kupata vibali, hali ambayo ilikuwa inawakatisha tamaa wawekezaji kuwekeza hapa nchini," alisema na kuongeza kuwa Baraza litaendelea kusimamia kanuni, sheria na taratibu za mazingira.

Dk. Gwamaka amesema kuwa, elimu kwa wananchi pamoja na mafunzo kwa maofisa mazingira yataendelea kutolewa, ili kufikia malengo ambayo serikali yao imejiwekea.



Ofisa Biashara Mwandamizi wa Benki ya ACB, David Korosso (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu benki hiyo kuanza kutoa huduma za malipo ya serikali na makusanyo ya kodi zote zinazolipwa kwa Mamlaka ya Mapato nchini, (TRA) kupitia mfumo wa kielektroniki. Wengine ni Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa benki hiyo, Dola Saria (kushoto) na Meneja wa benki hiyo, anayeshughulikia taasisi za serikali, Fatuma Kigembe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Lipumba kuwapa soko wakulima wa tumbaku

**Na Boniface Gideon,** TABORA

MGOMBEA urais kwa tiketi ya Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba, amesema iwapo atapata ridhaa ya kuongoza nchi, atahakikisha anasimamia na kuwatafutia masoko ya kimataifa wakulima wa tumbaku.

Amesema, kipaumbele kitakuwa soko la China kwa kuwa taifa hilo linaongoza duniani kwa kuwa na watumiaji wengi wa tumbaku, ambao ni zaidi ya milioni 400.

Akizungumza katika mkutano wa kampeni katika viwanja vya Igalula Station Kata ya Igalula, wilayani Uyuwi mkoani Tabora, Prof. Lipumba alisema mkoa huo unasifika kwa kulima zao la tumbaku, lakini wakulima hao wamewasahaulika kupewa kipaumbele, hali iliyowafanya kuendelea kuwa maskini kutokana na serikali kushindwa kuwatafutia masoko makubwa ya kimataifa, ambayo yanaushindani mkubwa wa bei.

Prof. Lipumba alisema, wakulima wanahitaji kupata serikali itakayosimamia maendeleo ya uchumi na itakayowekeza kwenye sekta ya kilimo kwa kujenga mazingira mazuri ya biashara, ili viwanda vya tumbaku viendelee kuwapo pamoja na kukuza soko lake. "Ndugu zangu, tumbaku ina madhara yake, lakini wavutaji bado wapo wengi zaidi ya Wachina milioni 400 wanavuta sigara, Tanzania yote watu wote tupo kama milioni 58, lakini wavuta sigara China ni mara saba ya wananchi wote waliopo," alisema na kuongeza:

"Tanzania pana soko la tumbaku, lazima tuwe na serikali itakayochangamkia soko hilo, wakulima wapate bei inayopatikana kwenye soko la tumbaku."

"Wakulima wa tumbaku wameharibiwa soko lao la tumbaku, sasa hivi hakuna kabisa mfano, mwaka jana kuna wakulima wengi walihifadhi tumbaku zao kwenye mabanda kwa sababu soko la tumbaku limeharibiwa na serikali ya CCM," alidai Prof. Lipumba.

Aliongeza kuwa, kampuni iliyokuwa na tumbaku imetozwa kodi na ushuru mpaka ikashindwa kuendeleza na kujiendesha, hivyo wakafunga viwanda.

"Nimefika Morogoro juzi watu wanalalamika hawana ajira, viwanda vilivyokuwa vikichambua na kusindika tumbaku vimefungwa," aliongeza.

Aliongeza kuwa, makampuni yaliyokuwa yakinunua tumbaku hivi sasa hayana soko kwa kuwa walikuwa wakipeleka kwenye makampuni yaliyokuwa na viwanda vya tumbaku, ambavyo hivi sasa vimefungwa, hali iliyosababisha makampuni hayo kushindwa kununua tumbaku.

"Wakulima wapo hoi pamoja na shuruba ya kilimo cha tumbaku, lakini sasa haina soko, biashara yake haitoki ...unaweza kuwa Igalula hapa, lakini njaa tupu mzunguko wa pesa hakuna, vijana hawana hela wanaweza kuona vitumbua vinauzwa mate yakawatoka, wanaishia tu kuangalia pesa hawana," alisema Prof. Lipumba.

Aidha, Prof.Lipumba aliwashauri wakulima na serikali kuacha kuendeleza zao la tumbaku pekee bali wapate mazao mbadala kama korosho, ambayo inaonekana kukubali kwenye ardhi ya Tabora, hivyo akipatiwa ridhaa atahakikisha anaweka utaratibu wa kuwa na kilimo cha korosho, kwa kuwa soko lake linauhakika zaidi.

# Mgaywa wa SAU kuondoa kodi ya ardhi

**Na Yasmine Protace**

MGOMBEA urais kupitia Chama cha SAU, Muttamwega Mgaywa, amesema kuwa akifanikiwa kushinda urais atahakikisha anaondoa kodi ya ardhi, ambazo zimekuwa ni kero kwa wananchi.

Pia serikali yake itawaondolea kero wananchi ambao, wanatumia kivuko cha kwenda Kigamboni, jijini Dar es Salaam, watasafiri bure.

Alisema serikali yake itahakikisha huduma za maji zinawafikia wananchi wote, na kuwa aliyefungiwa bomba atapata huduma hiyo bure na wale ambao walilipia huduma hiyo ni wale ambao, wanakuwa wanafanya biashara ya kuuza maji. Mgombea huyo aliyasema hayo, katika mkutano yake iliyofanyika katika maeneo ya Kigamboni na Tabata Degrees, jijini Dar es Salaam.

"Serikali yetu ina mipango mizuri, kupitia ilani yetu tutahakikisha tunayasimamia yote tuliyoyasema katika kuomba kura kwa wananchi," alisema Mgaywa.

Alisema, akiingia madarakani ataondoa magereza ya wilaya na kubakiza ya mkoa.

Alisema katika kuwainua kiuchumi wajasiriamali, atahakikisha wanapatiwa mikopo isiyo na riba na kuwa watapatiwa fedha.

Alisema benki ya wajasiriamali itaanzishwa, ili kutoa fursa ya kuwainua kiuchumi. "Tanzania watu wake wana akili sana, lakini changamoto waliyonayo pamoja na kuwa na akili, hawana mitaji," alisema Mgaywa.

Alisema katika kuhakikisha mitaji wanapatiwa, ndio maana wanataka kuanzishwa kwa benki ya wajasiriamali ambayo haitakuwa na riba.

Alisema, ili kuyatimiza hayo, wananchi wanatakiwa kumpa kura.

## Mabula kutatua kero wajawazito

**Neema Emanuel,** MWANZA

MGOMBEA ubunge kupitia Chama Cha Mapinduzi CCM, Jimbo la Ilemela, Angelina Mabula, ameahidi kutatua kero ya wanawake wanaojifungua na kukosa sehemu ya kupumzikia katika hospitali mbalimbali baada ya kujifungua.

Alitoa ahadi hiyo, kwenye kampeni zake katika Kata ya Kahama, kwenye mkutano wa hadhara na kueleza kuwa, atafanikisha ujenzi wa jengo la kupumzikia mama na mtoto baada ya kuzaliwa, huku akimtaka mgombea udiwani wa kata hiyo kwa tiketi ya CCM, Samuel Mita, kulichukulia kipaumbele suala hilo, atakapoingia kwenye halmashauri.

Mabula alisema, ujenzi wa jengo hilo utasaidia mama na mtoto kupata huduma hiyo bila shida, huku akiwapongeza wakazi wa Kata ya Kahama hasa mtaa wa Lukobe, kwa kufanya kazi kubwa ya kujenga zahanati kwa nguvu zao na kusaidiana na wadau na washirika wa maendeleo kutoka Canada.

"Nimepokea kimemo, wanasema wanahitaji jengo lingine liongezwe pale, nikuhakikishie Mita ukifika huko anza kulidai hilo, ili zahanati hiyo iweze kujengewa jengo la kinamama kupumzikia wanapoenda kliniki na kipaumbele kiwe ni kuweka jengo la mama na mtoto, ili waweze kupata huduma hiyo bila shida," alisema Mabula na kuongeza:

"Lakini nyie pia ni mashahidi, kama mnakumbuka wakati tunaingia madarakani hakukuwa na hospitali ya wilaya, lakini sasa hivi tunayo."

Aliongeza kuwa, akipatiwa ridhaa atajikita kufanya mambo mbalimbali yakiwamo kutatua migogoro ya ardhi katika sekta ya ardhi, upimaji wa viwanja, sekta ya barabara, umeme, maji, elimu, mikopo sambamba na miradi ya kimkakati.

Mabula ambaye ni Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, pia aliwaomba wavuvi kutumia fursa hiyo, ili kukuza uchumi wao. Kwa upande wake, naye Mita anaeleza kuwa ujenzi wa jengo la mama na mtoto atalipa kipaumbele.

"Nikiingia madarakani wananchi wangu watarajie mambo makubwa sana, sitowaangusha...nitahakikisha miradi inayokuja Kahama, nitaisimamia kikamilifu," anaeleza Mita.

# Bil. 6/- zatumika miradi ya maji Mkalama

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imetumia zaidi ya Sh. bilioni 6.318 kwa ajili ya ujenzi wa miradi kwenye vijiji mbalimbali vya wilaya ya Mkalama, mkoani Singida ili kuwaondolea adha ya majisafi wananchi wake.

Hayo yalisemwa juzi na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, wakati akizungumza na wananchi waliohudhuria mkutano wa kuwanadi wagombea ubunge na udiwani wa CCM uliofanyika kwenye viwanja vya stendi ya mabasi Gumanga, wilayani Mkalama.

Mheshimiwa Majaliwa ambaye alikuwa mkoani Singida kumuombea kura mgombea urais kwa tiketi ya CCM, Dk. John Magufuli, alisema serikali ya awamu ya tano imejenga miradi ya kimkakati zaidi ya 1,490 kwenye sekta ya maji nchi nzima.

Akifafanua baadhi ya miradi iliyofanyika katika kipindi cha mwaka 2015/2016 na 2019/2020, Mheshimiwa Majaliwa alisema kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 1.37 zimetumika kwa ajii ya mradi wa maji vijiji vya Mughano, Ngimu, Mgori, Malolo, Kijota, Ghaluyangu na Mangida.

"Miradi mingine ni mradi wa maji kijiji cha Mwankoko 'B' ambao umetumia Sh. milioni 656, na mradi wa maji kijiji cha Kisaki ambao umetumia Sh. milioni 551. Pia shilingi milioni 428 zimetumika kwa ajili ya mradi wa usambazaji wa maji kijiji cha Gumanga na shilingi milioni 910 zimetumika kwa ajili ya mradi wa usambazaji wa maji kijiji cha Nyahaa," alisema.

Akifafanua zaidi, Majaliwa alisema Sh. milioni 341 zimetumika kwa ajili ya mradi wa uchimbaji wa visima virefu saba katika maeneo ya Nduguti, Kisuluiga, Matongo, Ipuli, Mkiko, Mwanga, Wangeza, Kinampundu, Kinyangiri, Msingi, Senene, Milade, Mbigigi, Nduguti (visima viwili), Tumuli (kisima kimoja) na Ibaga (kisima kimoja).

Alisema Sh. milioni 158 zimetumika kwa ajili ya mradi wa uboreshaji maji katika kijiji cha Nduguti na Sh. milioni 70 zimetumika kwa ajili ya uboreshaji maji katika kijiji cha Kinyangiri.

Mbali ya juhudi zote hizo, Majaliwa alisema Sh. bilioni 1.37 zimetumika kwenye mradi wa maji kwa vijiji 10 vya Ibaga, Lyelembo, Mpambala, Ikolo, Kinyambuli, Ipuli, Makuro, Donimic, Ishinsi Nkalalala na Lukomo.

Wakati huohuo, Majaliwa alisema Sh. milioni 235.98 zimetumika kwa ajili ya uchimbaji wa visima virefu na vifupi 20 ikiwa ni pamoja na ufungaji wa pampu za mkono. Alisema kiasi kingine cha Sh. milioni 144 kimetumika kwa ajili ya upanuzi wa mradi wa maji kijiji cha Mntamba na sh. milioni 85 nyingine zimetumika kwa ajili ya ukarabati wa mradi wa maji kijiji cha Ipuri.




Dk. Mashaka Massod wa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Morogoro, akimfanyia uchunguzi mkazi wa Malinyi, Hamza Hassan, kabla ya kufanyiwa upasuaji wa mtoto jicho, katika kambi maalum ya utoaji huduma hiyo, bure chini ya udhamini wa Taasisi ya HAK, Humanitarian Aid Association ya nchini Uturuki, iliyofanyika hospitalini hapo, wikiendi. Wagonjwa 200, wamefanyiwa upasuaji katika kambi hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# World Vision yapewa tano kambi za usomaji

**Na Shaban Njia,**

WANANCHI wa kata za Kilango na Iyenye Halmashauri ya Mji wa Kahama mkoani Shinyanga, wamelipongeza Shirika lisilo la kiserikali la World Vision Tanzania kwa kuanzisha makambi ya usomaji ambayo yameongeza uelewa kwa wazazi katika ufuatiliaji wa wanafunzi wanaosoma katika shule za msingi.

Makambi hayo yalianzishwa tangu mwaka jana na shirika hilo katika kata za Kilago na Iyenze lengo likiwa ni kuwaongezea uwezo wazazi namna ya ufuatiliaji wa masomo kwa watoto wao wa shule za msingi sambamba na kuwaandaa watoto wenye umri wa kwenda shule kujua kusoma na kuandika.

Waliyabainisha hayo jana walipotembelewa na mwezeshaji wa mradi wa elimu Kilago Iyenye kutoka World Vision Tanzania, Lwitiko Philipo, wakati wa ukaguzi wa makambi hayo ambayo yamejengwa kwa nguvu za wananchi.

Betha Phabiani, mkazi wa Kata ya Kilago, alisema kabla ya kuanzishwa kwa makambi hayo, wanafunzi wengi walikuwa wakimaliza elimu ya msingi wakiwa hawajui kusoma na kuandika na wengi wao walikuwa wanafunzi wa kike ambao walitumia muda mwingi kwenye kazi za nyumbani.

Nae William Madata, Mwenyekiti wa Kitongoji cha Ngudu Kata ya Kilago, alisema,katika ujenzi wa makambi hayo waliuza mazao ya kijiji maguni 25 ya mpunga kwa kiasi cha shilingi milioni 1.5 na kujenga kambi ambayo imewapati fursa wanafunzi kujua kusoma na kundika kabla ya kuanza darasa la kwanza.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Iyenze, Neema Chiloloma, alisema kwa sasa inawarahishia kazi ya kufundisha baada ya uwepo wa makambi hayo.

# Umeme kuipaisha wilayaTanganyika

**Na Neema Hussein,** KATAVI

MKUU wa Wilaya ya Tanganyika mkoani Katavi, Saleh Mhando, amesema mpango wa Serikali kupeleka huduma ya umeme katika kila kijiji wilayani humo utasaidia kuboresha hali ya maisha kwa wananchi na kuchochea kukua kwa uchumi wa wilaya hiyo.

Mhando alisema hayo kwa nyakati tofauti, wakati wa ziara yake katika vijiji vya Mwese, Lugonesia na Lwege kukagua na kuhimiza shughuli mbalimbali za maendeleo zinazofanywa na serikali kwa kushirikiana na wananchi.

Alisisitiza kuwa, Serikali imekusudia kupeleka huduma ya umeme kwa kila mwananchi pamoja na taasisi za umma kama shule, zahanati, masoko, nyumba za ibada, vituo vya polisi na ofisi nyingine za serikali ili kurahisisha na kuchochea utoaji huduma bora kwa wananchi.

Aidha aliwaeleza wananchi kwamba mradi wa umeme vijijini (REA) hauna fedha za kulipa fidia kwa mazao yatakayokatwa kupisha mradi huo na kuwataka wananchi kufanya mandalizi ya kupokea umeme huo.

# Mgombea CHADEMA aahidi gari la zimamoto

**Na Thobias Mwanakatwe**

MGOMBEA ubunge Jimbo la Kyela kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Alinanuswe Mwalwage, amesema kama wananchi watampa ridhaa atahakikisha Wilaya ya Kyela inapata gari la zimamoto.

Akizungumza na wananchi kwenye mkutano wa kampeni uliofanyika juzi kata ya Mbugani, alisema ni jambo la kushangaza tangu wilaya hii ianzishwe mwaka 1972 haijawahi kupata gari la zimamoto.

Alisema kutokana na kukosekana kwa gari la zimamoto, matukio ya moto yanapotokea imekuwa changamoto kubwa kuweza kudhibiti moto, ambapo wananchi wanalazimika kujitolea kuzima wenyewe pengine bila mafanikio.

Mwalwage alitoa mfano wa tukio la kuungua moto wodi ya wazazi katika Hospitali ya Wilaya ya Kyela lililotokea Septemba 11, mwaka huu, ambapo wananchi walilazimika kujitolea kuzima moto huo japo baadhi ya vitu viliteketea. "Kwanza tunawashukru sana wananchi wa Kyela mjini kwa jinsi walivyojitolea kwanza kuokoa maisha ya wagonjwa waliokuwa wamelazwa katika wodi ile na pia kwa kufanikiwa kuudhibiti moto usiweze kuleta madhala zaidi katika majengo mengine," alisema. Alisema ni jambo la kushangaza makao makuu ya wilaya kukosa gari la zimamoto wakati kuna taasisi kubwa kama benki na nyinginezo ambapo kukitokea tatizo la moto hadi gari liangizwe kutoka Mbaya Mjini ambapo linaweza kutumia zaidi ya saa tatu hadi kufika Kyela Mjini.

Mwalwage pia aliwaeleza wananchi kuwa wakimchagua atadhibiti tatizo lililoanza kujitokeza katika wilaya hiyo la wafanyabiashara kutozwa faini kubwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na hivyo kusababisha wengine kushindwa kuendesha biashara zao.

Kuhusu vitambulisho vya wajasiriamali, alisema utaratibu uliowekwa siyo mzuri kwani wapo wajasiriamali ambao kupata shilingi elfu 20 kwa mwezi ni kazi sasa wanapoambiwa watowe kwa ajili ya vitambulisho ni kuwaonea.

ama
ALHAMISI SEPTEMBA 17, 2020
AFYA NA MAZINGIRA




Ukurasa 12

**Mazoea ya kubana haja ndogo hayajamwacha salama anayeizuia**



Ukurasa 13

Vijiji Handeni vyachangamkia hifadhi za misitu kwa kasi



Ukurasa 14

**Yanayoikwamisha Kigoma kutumia nyota ya kijani**

AFYA

**Na Christina Mwakangale**

# HABARI MBAYA

## •Selimundu inatisha,Tanzania ya tano wingi wagonjwa duniani
## •Milioni 10 wana nasaba, wengi Kanda ya Ziwa

SELIMUNDU ni ugonjwa wa kurithi unaosababisha seli nyekundu za damu kuwa na umbo la nusu mwezi (mwezi mchanga) badala ya duara au mviringo.

Ni matokeo ya mabadiliko yasiyo ya kawaida yanayotokea katika chembe nyekundu za damu na kuzikwamisha kupita kwenye mishipa midogo midogo ya damu.

Kawaida chembe nyekundu zina umbo la mviringo linaloziwezesha kupita kwenye mishipa midogo ya damu na kusafirisha hewa ya oksijeni sehemu mbali mbali mwili, anaeleza Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi zinazojishughulisha na ugonjwa wa selimundu (TANSCDA), Dk. Deogratius Soka.

Anasema ugonjwa huo ni mwingi nchini na unachangia vifo vya watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano kwa asilimia 6.7.

Ikimaanisha kuwa kati ya watoto 10 sita mpaka saba wanaozaliwa na ugonjwa huo hufariki dunia.

Mtaalamu huyo anafafanua zaidi kuwa mwenye selimundu seli nyekundu za damu zinakuwa na umbo la mwezi mchanga na huishi kwa muda mfupi kati ya siku 10 hadi 20, ikilinganishwa na zile za asiye na maradhi zinazoishi siku 90 hadi 120.

Anasema seli zinapoishi muda mfupi, husababisha upungufu wa kudumu wa damu mwilini ambalo kitabibu huitwa chronic anaemia (anemia sugu).


"Kutokana na umbo la nusu duara chembe nyekundu za 'sickle cell' hukwama katika mishipa midogo ya damu na kuziba mzunguko wa wake pamoja na wa oksijeni mwilini," anasema Dk. Soka.

**DALILI ZA UGONJWA**

Anazitaja Dk Soka kuwa ni pamoja na maumivu makali, kiharusi, maambukizi ya magonjwa na hata kuharibika kwa ogani mbalimbali mwilini.

**SABABU ZA UGONJWA**

Dokta Soka anaeleza kuwa ugonjwa wa selimundu ni wa kurithi, kwa njia zile ambazo mtu hurithi rangi ya ngozi au macho na kimo hivyo kwa njia hizo huzaliwa na ugonjwa huo.



"Vinasaba vya selimundu hurithiwa kutoka kwa wazazi wote wawili baba na mama na mtoto hawezi kupata selimundu kwa kuambukizwa kama vile kuishi na kushirikiana kwa ukaribu wenye ugonjwa huu."

Kwa mfano, anasema huwezi kupata kwa kula, kucheza au kulala na mtu mwenye siko seli.

**TANZANIA YA TANO DUNIANI**

Mtaalamu huyo anasema selimundu huathiri mamilioni ya watu duniani kote hususan wanaoishi Afrika Kusini ya Sahara.

Anasema takribani watoto 300,000 hadi 500,000 wenye siko seli huzaliwa kila mwaka duniani, kati yao asilimia 70 wapo Kusini ya Sahara.

"Tanzania ni mojawapo kati ya nchi zenye wagonjwa wengi wa selimundu duniani inakadiriwa kuwa kati ya watoto 8,000 hadi 11,000 huzaliwa na ugonjwa huu kila mwaka.

Inakadiriwa kuwa asilimia 15 hadi 20 ya watu wote nchini wana vinasaba vya ugonjwa wa selimundu 'sickle cell traits'.

Anabainisha kuwa Tanzania ni kati ya nchi zilizoathiriwa na ugonjwa huo duniani, ikiwamo Nigeria, India na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na kwamba kila watoto wanane kati ya 1,000 wanazaliwa na ugonjwa huu.

***ATHARI KIAFYA***

Huleta maumivu makali mwilini kutokana na chembe nyekundu za selimundu kushindwa kupita kwa urahisi katika mishipa midogo ya damu.

Pia watoto hupata maambukizi ya vimelea vya magonjwa mbalimbali kama vichomi (pneumonia), homa ya uti wa mgongo na ya ini.

Kadhalika, Dk. Soka anasema wenye ugonjwa wa selimundu wana upungufu wa damu, kutokana na chembe nyekundu kuishi muda mfupi.

Anaeleza kuwa hali hiyo husababisha mgonjwa wa selimundu kuwa katika hatari ya kupata upungufu mkubwa wa damu wakati wote.

"Kuvimba kwa mikono na miguu, mara nyingi kunakoambatana na homa, hali hii husababishwa na chembe nyekundu za selimundu kukwama na kuziba mzunguko wa damu kwenda kwenye mikono na miguu," anaeleza Dk. Soka.

Anasema wagonjwa wa selimundu hubanwa na kifua kutokana na kukwama na kuziba kwa mzunguko wa damu inayokwenda mapafuni.

"Mara nyingi ugonjwa husababisha matatizo ya kupumua, dalili zake ni maumivu ya kifua, kukohoa, homa na kupumua kwa shida."

Pia, anasema watu wazima hupata kiharusi kutokana na kukwama na kuziba mzunguko wa damu kwenda kichwani na kusababisha kiharusi ambacho humletea mgonjwa ulemavu na matatizo ya uelewa na kumbukumbu.

**TIBA**

Dk. Soka anasema matibabu ya selimundu ni kupunguza madhara ama dalili zitokanazo na ugojwa huo, kama vile kutibu na kuzuia maumivu, kuzuia vimelea vya magonjwa, upungufu wa damu na kiharusi.

"Hakuna tiba mahususi kwa wagonjwa wa selimundu, hivyo matibabu hutofautiana kutokana na dalili mfano kuongezwa damu au maji mwilini na dawa za maumivu.

Hadi leo tiba pekee ya ugonjwa

Endelea Uk. 12

AFYA

# Mazoea ya kubana haja ndogo hayajamwacha salama anayeizuia

**Na Sabato Kasika**

IMEKUWA ni kawaida kwa baadhi ya watu kuvumilia kuwa kwa saa kadhaa haja ndogo. Akiwa safarini au sehemu anayoona kuwa hawezi kujisaidia kwa amani anakaa kwa muda mrefu na kuupuuza haja hiyo.

Tatizo hilo wakati mwingine husababishwa na mambo mengi kama kukosa eneo la kujisitiri, gharama ya choo ambayo ni Sh. 500 kwa Dar es Salaam, uchafu wa vyoo, kukosekana maji au tishu na wakati mwingine kupuuza.

Lakini kwa mujibu wa wataalamu afya, kila mtu anatakiwa kujisaidia haja ndogo kila baada ya saa nne hadi sita na iwapo atavumilia, kwa muda mrefu atajiweka katika hatari ya kukumbwa na matatizo mbalimbali ya kiafya.

Wataalam wa afya wanataja baadhi ya madhara ambayo yanatokana na kuzuia mkojo kuwa ni pamoja na kujisaidia katika nguo baada ya kuzidiwa.

Daktari bingwa wa magonjwa ya ndani ya mwili wa binadamu (internal medicine) , Lucas Nzobendo, wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, anataja tatizo lingine kuwa ni kutanuka kibofu kuliko ukubwa wake.

Inaeleza :"Mtu anapokaa na haja ndogo kwenye kibofu kwa muda mrefu, unapatwa na maumivu makali, lakini maumivu hayo hutokomea mara tu unapokwenda haja ndogo. Maumivu hayo yanaweza yakawa ni mfumo wako wa maisha kama hutachukua tahadhari mapema."

Vilevile, Dk. Nzobendo, anaonya kuwa hatimaye, ni kupata mawe kwenye kibofu na figo, hali ambayo si salama na kwamba kubana haja ndogo kwa muda mrefu kunahatarisha afya ya kibofu.

"Pamoja na ushauri huo wa kitaalam, ninadhani kuja haja pia ya kuhakikisha kila sehemu kunakuwa na vyoo ya umma, watu wavitumie inavyotakiwa ili waepuke mtindo wa kubana haja ndogo." Anaeleza.

Anasema kuwa si kwamba hakuna vyoo vya umma, bali ni vilivyopo ni vichache, katika maeneo mbalimbali ya mijini na hata kandokando ya barabara kuu kwa ajili ya wasafiri wanaohitaji 'kuchimba dawa'.



Vyoo vichafu mijini vinaweza kuwa sababu ya watu wengi kulazimika kubana haja ndogo kwa muda mrefu. **PICHA: MTANDAO**

### HALI HALISI

Nipashe imegundua kuwa kwa mafano yapo baadhi ya masoko ambayo hayana vyoo na wakati mwingine hata stendi za daladala hazina, hali ambayo inawezekana inachangia kuwafanya watu kubana haja ndogo kwa muda mrefu.

Kwa mfano ukosefu wa vyoo kandokando ya barabara kuu kwa ajili ya wasafiri wanaokwenda maeneo mbalimbali inasababisha wengi kushindwa 'kuchimba dawa' hasa kinamama na wasichana ambao inakuwa vigumu kuingia vichakani ama sehemu ya wazi barabarani.

Baadhi ya abiria wanaliambia gazeti hili kuwa changamoto inakuwa kubwa zaidi kwa wanawake ambao wanakwama kutokana na ukosefu wa huduma za vyoo safi wakiwa safarini.

"Haja ndogo au kubwa inahitaji faragha, hivyo wapo baadhi ya watu, ambao hawawezi kujihudumia hadharani, badala yake wanajibana hadi wafike sehemu yenye faragha." Anasema abiria wa basi la Tilisho, Wema Marriott.

Wema anasema wengi wanaumizwa na mazingira, hivyo ni vyema kukawapo vyoo vya kutosha, visafi, vyenye maji na tishu ili waweze kujistiri kuliko watu kusafiri umbali wa kilometa nyingi bila kuwapo choo kandokando ya barabara.

Watalaama wa afya wanasema, kutokana na vyakula na vinywaji ambavyo watu hula, kibofu cha mkojo kinaweza kujaa haja ndogo mapema na unapofikia karibu mililita 50 hadi 500 mtu huanza kuhisi kwenda haja.

Wanasema, hiyo ni kutokana na kwamba, kibofu cha mkojo kimezungukwa na vigunduzi asili (receptors) vinavyopeleka taarifa katika ubongo kuonyesha kuwa kibofu kimekaribia kujaa au kimejaa.

Aidha, baada ya taarifa hizi kufika katika ubongo nao unatoa taarifa katika kibofu ili kiweze kishikilie mkojo huo kwa kuikaza misuli maalumu (sphincters) hadi hapo muda wa kwenda kujisaidia utakapofika.

Mtandao ya afya inaeleza kuwa wakati mwingine uwezo wa vigunduzi asili (receptors) vilivyoko katika kibofu cha mkojo vinaweza kupoteza uwezo wake tena wa kufanya kazi hizo iwapo mtu ataendelea kubana haja ndogo.

Vilevile wale wanaozembea ama kupuuzia kwenda kujisaidia haja ndogo, wanakumbushwa na wataalam wa afya kuwa hali hiyo pia husababisha ubongo kupata usumbufu wa taarifa za kujaa kwa kibofu cha mkojo.

Ni vyema wale ambao huzembea wakajifunza ili waachane na mtindo huo, kwani wakiendelea kuubana kwa uzembe ama kukosa sehemu ya kujisaidia watambue hawako salama.

Hivyo, suala la kuwapo vyoo vya umma vya kutosha ni muhimu kwa ajili ya kupunguza idadi ya watu wanaobana haja ndogo, kutokana na kukosa sehemu ya kujistiri, lakini si kwa wale wanaozembea.

# HABARI MBAYA

Inatoka Uk. 11

huu ni kuwekewa uboho (bone marrow) au kupandikizwa kiini kwenye shina la mfupa kunakozalishwa damu. anasema Dk. Soka.

Anaeleza kuwa tiba hiyo hufanywa kwa kuchukua urojo wa mifupa kutoka kwa mtu asiye na selimundu na kupandikiza kwenye mifupa ya mgonjwa.

Anafafanua kwamba, tiba hiyo husaidia mifupa ya mwenye selimundu kuzalisha chembechembe za damu zilizo nzima na si zilizo nusu yaani zenye umbu la mwezi.

"Tanzania iko kwenye mchakato wa kuhakikisha huduma hizi za upandikizaji wa uboho zinapatikana nchini," anasema.

### UNYANYAPAA

Akizungumzia unyanyapaa anasema kuna dhana potofu kwenye jamii ambazo zinasababisha wagonjwa wa selimundu kunyanyapaliwa.

"Dhana iliyopo ni kwamba watu wanaoishi na ugonjwa huu hawawezi kuishi zaidi ya umri wa miaka 18.

Ukweli ni kwamba hakuna ukomo wa kuishi kwa watu wanaoishi na selimundu, wanaweza kuishi zaidi ya miaka 18.

Kuna watu wengi sana waishio na selimundu wenye umri zaidi ya miaka 18," Anabainisha Dk. Soka na kueleza kuwa wanaougua selimundu wanaweza kufurahia mapenzi pasipo tatizo na vile vile wanaoa na kuolewa na kupata watoto.

### NI TISHIO NCHINI

Kaimu Mkurugenzi wa Tiba Wizara ya Afya, Dk. Sarah Maongezi, anasema watoto 100 walio chini ya umri wa miaka mitano, hufariki kila mwaka nchini kwa ugonjwa huo.

Dk. Maongezi anasema hayo hivi karibuni jijini Dodoma, akifungua semina kwa wanahabari kuhusu ugonjwa wa selimundu na kwamba, Tanzania ni ya tano duniani na ya nne Afrika kuwa na wagonjwa wengi wa selimundu .

Anasema idadi hiyo kubwa na wagonjwa wengi hutokea mikoa ya Kanda ya Ziwa na kwamba sababu hazijafahamika.

Mratibu Mratibu wa Selimundu wa wizara hiyo, Dk. Asteria Mpoto, anasema serikali inafanya uhamasishaji wa kufahamika tatizo hilo na kwamba kila mwaka, Septemba Mosi hadi 30 ni mwezi wa kuelimisha jamii kuhusu ugonjwa wa selimundu.

MAZINGRA

# Vijiji Handeni vyachangamkia hifadhi za misitu kwa kasi

**Na Beatrice Philemon**

BAADA ya kuona kuwa misitu ya hifadhi ya vijiji huongeza mapato yanayotokana na miti, mkaa, mbao na magogo kwa ajili ya shughuli za uhifadhi, hivi sasa wanavijiji wa Madebe na Kang'aka mkoani Tanga wameanza kutenga maeneo ya uhifadhi wa msitu

Hayo yanabainika wakati wa ziara ya wanahabari waliotembelea vijiji hivyo kufuatilia manufaa yaliyopatika kwenye mafunzo yaliyotolewa na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) kwa lengo la kuanzisha misitu ya hifadhi ya kijiji.

Wanavijiji wanapewa mafunzo ya kuhifadhi misitu kwa lengo la kuanzisha misitu ya hifadhi za vijiji kwa kutumia Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Jamii (USMJ) na uvunaji endelevu yanayosimamiwa na MJUMITA).

Hivi sasa kila kijiji chenye msitu wa asili ambao haujarasimishwa kinashauriwa kiutenge kuwa msitu wa hifadhi wa kijiji na kuusimamia kikamilifu kwa ajili ya maendeleo yao na ya wanakijiji kwa lengo la kupunguza uharibifu wa maliasili hiyo .

Lengo la USMJ ni kusaidia wananchi kuhifadhi misitu na kunufaika na rasilimali zilizopo katika ardhi ya vijiji .



Mwenyekiti wa Kijiji cha Madebe, Kassimu Bakari, akionyesha eneo lililotengwa kuwa hifadhi ya misitu ya asili ili kulinda vyanzo vya maji vinavyokauka kutokana na uharibifu wa misitu kwenye mlima wa Kwa Lugulu. **PICHA: BEATRICE PHILLEMON.**

Uzoefu wa wadau wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Jamii unaonyesha kuwa misitu ya vijiji yenye kutumia utaratibu wa uvunaji endelevu hutoa motisha kwa serikali za vijiji na jamii kusimamia misitu kikamilifu na wakati huo kuchangia maendeleo ya wananchi.

Akizungumza na Nipashe, wakati wa ziara hiyo Mwenyekiti wa Kijiji cha Madebe, kilichoko kata ya Kang'aka, Kasim Bakari, anasema kijiji kimetenga hekta 2,564 za msitu katika pori la Mkuzi kwa ajili ya kuufanya msitu wa hifadhi wa kijiji na usimamizi shirikishi wa misitu kwa jamii.

Mbali na hilo pia wanataka kutenga eneo katika mlima wa Kwa Lugulu na Mbuzini kwa ajili ya kulinda vyanzo vya maji ambavyo hivi sasa vimeanza kukauka kutokana na uvunaji holela wa miti, mbao pamoja na mkaa.

"Tayari tumeishakaa kikao cha awali na watalaamu na kuamua wapi tuweze kuhifadhi na kupanga sehemu ya malisho. Ila mkutano wa wananchi bado haujafanyika, Jumanne tutakaa vikao na wanavijiji ili kujadili suala hili," anasema Bakari.

Anaeleza kuwa ingawa wametenga eneo la uhifadhii, bado kuna uharibifu katika eneo la mbuzini .

"Wananchi waliozuiliwa katika eneo la Mbuzini na Kijiji cha Msaje na kwa Magome kwa ajili ya makazi wanaongoza kuharibu misitu yetu ya asili kwa kukata miti ovyo," anawaonya.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Madebe, Hassan Mbwego anasema kijijini hapo kuna maliasili nyingi za misitu ya asili ikiwamo milima ambayo inaweza kutumika kwa shughuli za utalii lakini hazipo kwenye mpango wa kuhifadhiwa kisheria.

"Kama misitu yetu ingehifadhiwa kisheria tungepata mapato kupitia kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo," anasema Mbwego

Anaeleza kuwa wananchi wanaomba halimashauri iwasaidie ili wahifadhi msitu na kijiji kianze kunufaika.

Mbali na hilo hivi sasa wafanyabiashara wa mbao kutoka maeneo mbalimbali wameanza kuingia usiku kwenye msitu na kukuta miti kwa ajili ya mbao.

Wafanyabiashara hawa wameamua kutumia nafasi hiyo kwa sababu msitu wao bado haujahifadhiwa kisheria na hilo linachangia kwa kiasi kikubwa kushindwa kuwakamata na kuwachukulia hatua watuhumiwa.

"Sisi wanakijiji tunaomba Halmashauri ya Wilaya ya Handeni itusaidie ili tuweze kuuhifadhi na kuumiliki kisheria msitu wetu kwa sababu unaweza kumkamata mtuhumiwa lakini huwezi kumfanya lolote," anasema.

Mbali na hilo, anasema eneo la msitu lililotengwa kwa ajili ya shughuli za uhifadhi lina changamoto ya wafugaji, wakulima na wachoma mkaa wanaoendelea kuharibu msitu huo.

"Tunaomba serikali itusaidie watu hawa waondoke ili tuweze kuhifadhi msitu wetu kwa ajili ya maendeleo ya kijiji chetu na kwa manufaa ya sasa na ya kizazi kijacho," anasema Mbwego.

Anaeleza kuwa ingawa kijiji chao kimebarikiwa kuwa na rasilimali misitu, bado hakipati ushuru kutokana na rasilimali hizo.

Anaeleza kuwa Kijiji cha Madebe kimeanza mwaka 1976 na kina wakazi 6,000.

Akizungumzia mafanikio ya mafunzo juu ya uhifadhi misitu Mjumbe wa Halmashauri ya Kijiji cha Madebe, Philipo Abdallah, anasema mafanzo yamefungua macho kwenye kuhifadhi misitu kwa ajili ya maendeleo yao.

"Hapo awali tulikuwa hatujui faida za misitu, sasa tumezijua kuwa ni mali ya kijiji ndiyo maana tumekubali kutenga eneo kwa ajili ya uhifadhi ambao utatuwezesha kupata fedha za miradi ya maendeleo hapa kijijini," anasema mjumbe huyo.

Anaeleza kuwa kupitia utunzaji wa misitu watakuwa na maendeleo na kama wakishirikiana na halmashauri na wadau wengine kama MJUMITA, Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili (TFCG) WWF- Tanzania watapata mafanikio makubwa.

Mjumbe wa Kijiji cha Madebe, Hawa Aziz anasema kutokana na uharibifu wa vyanzo vya maji uliosabishwa na kukata miti milima ya Kwa Lugulu na Mbuzini wananchi wanatumia maji ya visima yasiyo salama.

"Chanzo cha maji cha Kilembelo,Kijela, Lujorozi na Maturi ni baadhi ya vyanzo vinavyoanza kukauka baada ya uharibifu wa misitu ya asili kwa ajili ya mbao," anasema Hawa.

Ofisa Misitu Msaidizi, Halmashauri ya Handeni, Athuman Kambi, anawaambia wanakijiji :"Ni jukumu letu wanakijiji kujua wapi tutenge eneo la msitu wa hifadhi ya kijiji, tupahifadhi na kwanini tufanye hivyo, hii ni fursa ambayo hatuwezi kuipoteza."

Anaeleza kuwa wanakijiji cha Gole wataanza kupokea Sh. milioni 260 kwa ajili ya uvunaji endelevu.

"Tuamue kuhifadhi maeneo yetu bado hatujachelewa.Haya maeneo machache tukiyahifadhi vizuri hayawezi kuingiliwa kirahisi kwa ajili ya shughuli za uvunaji na sisi halmashauri tumekuja katika kijiji chenu ili tujue tufanyeje ili kuanza kuhifadhi misitu yenu," anasema

Revocatus Njau ni Ofisa Mawasiliano na Uraghabishi wa Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania, TFCG, anayesema kijiji cha Madebe ni moja kati ya hekta milioni 17.6 za misitu ambazo hazijahifadhiwa kisheria.

Anasema ni karibu asilimia 80 ya hekta milioni 22 za misitu iliyo katika ardhi ya vijiji.

"TFCG kwa kushirikiana na wadau, halmashauri ya wilaya tunafanya kampeni ya misitu ya hifadhi kwa kila kijiji ili kuboresha rasilimali hizi, kuhifadhi na kupata mapato kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya kijiji," anasema.

Anasema TFCG inajikita katika kampeni hiyo kuhimiza usimamizi endelevu wa misitu nchini kuziwezesha serikali za vijiji kunusuru takribani hekta milioi 17.6 za misitu ambazo hazijahifadhiwa kisheria katika ardhi zake.

"Tumetembelea Madebe na Kang'ata tumefurahi kuona wananchi wana mwamko na mikakati ya kuhifadhi misitu yao, tayari wameishatenga maeneo ya uhifadhi na usimamizi shirikishi wa misitu,"anasema Njau.

Madebe imetenga hekta 2,564 kuanzisha msitu wa hifadhi ya kijiji katika pori la Mkuzi ambalo halijapimwa.

Anapongeza hatua ya halmashauri kuanzisha shamba la miti kwa ajili ya mbao na kusema ni kuonyesha mfano kwa wenngine na TFCG inawapatia miche 6,000 ya miti kuunga mkono juhudi hizo.

Aidha, Kijiji cha Kitumbi kimehifadhi msitu wake kisheria na tayari kimeandaa mpango shirikishi wa hifadhi ya misitu wakati kijiji cha Kang'ata wameandika barua kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Handeni (DED) wakitaka kuhifadhi msitu wao.

AFYA

# Yanayoikwamisha Kigoma kutumia nyota ya kijani

**Na Pendo Thomas, KIGOMA**

UZAZI wa mpango au kufuata nyota ya kijani ni mbinu mbalimbali zinatumiwa kuwezesha kupata mtoto kwa muda uliopangwa au kupishanisha watoto kwa utaratibu wazazi wanaojiwekea.

Kupanga uzazi kuna njia kuu mbili za asili na za kisasa japo za asili ni ngumu kutokana na kuhitaji umakini mkubwa kwa vile uwezekano wa kufanikiwa ni chini ya asilimia 50, hivyo watu wengi wanaotegemea mbinu hizo wanaelezwa kuwa wanashindwa kufikia malengo ya kupishanisha watoto kama walivyopanga.

Ikumbukwe uzazi wa karibu karibu unadhoofisha afya ya mtoto kwa vile hatanyonya kwa miaka miwili kama inavyoshauriwa na wataalamu wa afya.

Aidha, anashindwa kumaliza miezi sita ya kunyonya ambayo inashauriwa asipewe chakula kingine tofauti na maziwa ya mama.

Lakini, njia za kisasa kama sindano, vipandikizi, kitanzi na vidonge zinatajwa kuwa na uwezekano kubwa wa kufanikisha mpangilio wa watoto kwa zaidi ya asilimiaya 95.

Mratibu wa afya ya uzazi na mtoto mkoa wa Kigoma Ernest Teyumwete, anasema mkoa huo uko chini katika matumizi ya njia za kisasa za kupanga uzazi ukilinganisha na malengo ya taifa ya kila mkoa kufikia asilimia 60 za matumizi ya njia hizo wakati kwa mwaka 2019 mkoa huo ukiwa na takribani asilimia 40 huku wilaya ya Uvinza ikiwa na asilimia 31 na manispaa ya Kigoma Ujiji asilimia 29.

Anasema uwiano wa serikali wa vizazi ni wastani wa 5.6 yaani watoto watano hadi sita tofauti na hali ilivyo kwa Mkoa wa Kigoma kwani uwiano huo kwa sasa ni 6.7.

Inamaanisha kuwa watoto sita hadi saba jambo linalosababisha wazazi wengi hasa wa vijijini kushindwa kumudu gharama za kuwahudumia watoto wao kiafya, elimu na chakula hivyo wengine kupata magonjwa yanayosababishwa na lishe duni kama udumavu na utapia mlo.

''Tumekutana na kina mama wenye vizazi 10 hadi 15 tena wakiwa wamepishanisha watoto wao kwa muda mfupi. Hii ni hatari kwa afya ya mama na mtoto, ''anasema Teyumwete.

**FIKRA POTOFU**

Anaeleza kuwa kiwango hicho kinasababishwa na nadharia mbalimbali katika jamii kuhusu matumizi ya njia hizo ambapo wanaume wanatajwa kuwa kinara wa kukwamisha mafanikio.

Wanaelezwa kuwa wanawazuia wenza wao hupata huduma ya kupanga uzazi kama kuwapatia vitisho vya kuwaacha endapo watatumia na kuacha kuzaa.



Watoto wakizaliwa bila kupishana wanaweza kukabiliwa na magonjwa, lisheduni, utapia mlo na udumavu. **PICHA: MTANDAO.**

Suala hilo pia linahusishwa na kikwazo cha mitazamo ya kidini na utamaduni wengi wanakichukulia kama kumpangia Mungu nini cha kufanya.

Na wanafananisha jambo hilo na uasi au uvunjaji wa maadili

Mratibu wa afya ya uzazi na mtoto Mkoa wa Kigoma , anasema mwanamke anapojifungua bila kupumzika inasababisha kizazi kuchoka na inaweza hatarisha usalama wa maisha yake pamoja na mtoto aliye tumboni.

Mkoa umeendelea kufanya jitihada za kuelimisha jamii kukuza uelewa chanya wa matumizi wa njia za kisasa za uzazi wa mpango ili kuwezesha watoto wanaozaliwa kupata haki ya kunyonya maziwa ya mama kwa miezi sita bila kuchanganya na chakula kingine pamoja na kunyonya kwa kipindi cha miaka miwili.

Wanatumia klinikI za baba mama na mtoto kutoa elimu hiyo kwa wenza wanaofika kupata huduma za afya ya uzazi ambapo maelezo muhimu na majibu ya maswali yanayo watatanisha yanapatiwa majibu kama sehemu ya kuondoa wasiwasi kwao huku wakati wengine wahudumu wa afya ngazi ya jamii wakihusishwa kutoa elimu hiyo kwenye maeneo yao, anasema.

> ‘Tumekutana na kina mama wenye vizazi 10 hadi 15 tena wakiwa wamepishanisha watoto wao kwa muda mfupi. Hii ni hatari kwa afya ya mama na mtoto, ''anasema Teyumwete.

Kutumia mfumo wa mkoba au wahuduma kwenda kuwafuata wahusika hasa vijijini ambao miundombinu ya kufika katika maeneo ya kutolea huduma hizo.

Anasema jamii inauelewa hasi juu ya matumizi hayo kwani baadhi yao wanahusisha huduma hiyo na uwezekano wa mwanamke kupata kansa ya shingo ya kizazi na ya kizazi, matiti na kupoteza uwezo wa kuzaa wakati.

Anasema endapo matumizi hayo yakifuatwa kama watalamu wanavyoelekeza ni muhimu kwa mwanamke kuondoa uwezekano wa kupata kansa.

Aidha jamii inapaswa kutambua lengo la matumizi ya njia za uzazi wa mpango si kumzuia mwanamke kuzaa bali kuwezesha kuwa na muda wa kupumzika na kupishanisha watoto wake angalau miaka miwili hadi mitatu.

Kufanya hivyo ni kuimarisha afya yake na kuepusha matatizo mengi wakati anapopata ujauzito mwingine kama mimba kutoka au mfuko wa uzazi kulegea.

Kutokana na ukinzani huo wapo wanawake wanaolazimika kutumia njia hizo kwa siri bila kushirikisha familia zao mbapo na wanachagua njia rafiki ambazo wenza wao hawawezi kuwabaini.

**WANAUME MIIBA**

Leonida Lenard, muuguzi katika kituo cha afya cha Ujiji, akizungumzia hali hiyo anaeleza kuwa waliwahi kupokea kesi kadhaa za wanaume waliofika katika kituo hicho wakilalamikia watoa huduma kuwapatia wenza wao njia hizo pasipo kuwashirikisha.

''Vipo visa vingi vya wanaume kuwaadhibu wenza wao baada ya kubaini kuwa wanatumia njia hizo mfano yupo baba mmoja aliongozana na mkewe kuja hapa baada ya kubaini anatumia njiti kupanga uzazi,''anasema.

Anasema mwanamume huyo kabla ya kufika kwa watoa huduma alikuwa anataka kukitoa kijiti hicho mkononi kwa kutumia kisu jambo ambalo linge hatarisha maisha ya mkewe.

Mage Nzalia mwanamama kutoka Wilaya ya Uvinza anasema ana watoto watano ambao waliozaliwa kwa tofauti ya mwaka mmoja na alipata ujauzito mtoto akiwa na miezi mitatu alipata ujauzito mwingine.

Anasema aliwahi kutumia njia za kisasa za uzazi wa mpango zilizo muwezesha kufanikiwa kwa muda lakini alishindwa kuendelea kuitumia kutokana na maudhi yaliyosababishwa na njia hizo.

''Baada ya kutumia nikawa nasikia vibaya pamoja na kuhisi maumivu wakati wa tendo la ndoa na nilipokwenda kuwaona watalamu wakanielekeza kubadilisha njia hiyo, hata hivyo niliogopa na kuamua kutumia mbinu za asili ambazo ukweli hazifanyi kazi,''anasema Mage.

**WANAUME WANASEMAJE?**

Mussa Mohamed mkazi wa Manispaa ya Kigoma Ujiji anasema hawezi ruhusu mke wake kujihusisha na njia za kisasa za kupanga uzazi na endapo akibaini anafanya jambo hilo kwa siri yuko tayari kumpatia talaka .

Anasema japo wataalam wa afya wanasema kuzaa karibu karibu kunasababisha watoto kuugua au kudumaa kutokana na kutonyonya lakini kwake si sababu ya kufanya aogope kwani atatumia dawa za asili kuwapa watoto wake.

Kutokana na athari za kiafya wanazoweza kuyapata wanawake kwa kuzaa karibu karibu taasisi na mamlaka zinazojishughulisha na afya ya uzazi zinapaswa kubadili mbinu za kukabiliana na changamoto hiyo kwa mikoa inayoshindwa kufikia wastani unaoelekezwa na serikali .

Kuliko kuwekeza nguvu zaidi kwa wanawake sasa elimu hiyo inawashirikishe wanaume kuliko wanawake kwani suala la kuzaa linajumuisha makubaliano ya pande mbili.

Licha ya kwamba wanawake ndiyo wanaozaa hutegemea zaidi mawazo ya wenza wao katika kuamua mambo ya watoto ndani ya ndoa.

Aidha, midahalo na semina mbalimbali kwa kundi hilo zitasaidia utatuzi wa changamoto tofauti na njia zingine kwani wahusika watapata nafasi ya kueleza wasiwasi wao kwa uhuru na kupatiwa majibu sahihi na wataalamu.



# Watanzania watakiwa kuepuka uagizaji vifaa vyenye kemikali

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imewataka Watanzania kuepuka kuingiza nchini kemikali na vifaa vinavyotumia kemikali zinazosababisha uharibifu wa tabaka la ozoni yakiwamo majokofu na viyoyozi vya mtumba.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, aliyasema hayo jana jijini hapa katika maadhimisho ya miaka 35 ya kuhifadhi tabaka la ozoni kwa manufaa ya afya ya binadamu na mazingira. Aliyasema hayo kwa niaba ya Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan.

Simbachawene alisema Tanzania imepunguza tani 216 sawa na asilimia 86 ya matumizi ya kemikali hizo na lengo ni kuondosha kabisa matumizi hayo ifikapo mwaka 2030. Aidha, alisema kumomonyoka kwa tabaka hilo kunachangiwa na matumizi ya baadhi ya kemikali katika majokofu, viyoyozi, vifaa vya kuzimia moto, usafishaji chuma, utengenezaji magodoro na viatilifu vinavyotumika kuhifadhi nafaka katika maghala. "Kumomonyoka kwa tabaka la ozoni husababisha madhara mbalimbali kwa afya ya binadamu na mazingira, kama vile saratani ya ngozi, uharibifu wa macho, athari za ukuaji wa mimea na viumbe vingine, hivyo ni muhimu kulinda tabaka ili kunusuru dunia dhidi ya athari hizi," alisema.

Simbachawene alisema ili kulinda tabaka hilo, Watanzania waingize vipoozi mbadala na rafiki kwa tabaka hilo na kununua bidhaa zilizowekwa nembo ya 'ozone friendly' ambayo inaashiria haikutengenezwa na kemikali zinazoharibu tabaka.

"Epukeni kutupa ovyo majokofu ya zamani ama vifaa vya kuzimia moto vyenye kemikali. Pia epuka matumizi ya kemikali za kufukiza udongo zinazoharibu tabaka, badala yake zitumike mbinu tunganishi za udhibiti wa wadudu waharibifu," alisema.

Awali, alisema miaka 35 iliyopita jumuiya ya kimataifa iliamua kuchukua hatua mahsusi ya kunusuru tabaka hilo kupitia mkataba wa Vienna, ili kulinda afya ya binadamu na mazingira yanayotokana na kumomonyoka kwa tabaka hilo.

Aidha, Simbachawene alisema baadhi ya kemikali mbadala zilizopendekezwa katika itifaki zimebainika kuchangia ongezeko la joto duniani na kusababisha mabadiliko ya tabianchi.

"Itifaki ya Montreal imefanyiwa marekebisho mara tano hadi sasa kutokana na ongezeko la orodha ya kemikali ambazo zina athari kwa tabaka la ozoni au ni rafiki wa ozone, lakini zinachangia mabadiliko ya tabia nchi, mabadiliko ya hivi karibuni yalifanyika Kigali, Rwanda ambayo yalilenga kuondoa uzalishaji wa kemikali ambazo zilikuwa mbadala," alisema.

Simbachawene alisema kupitishwa kwa marekebisho hayo kutachangia jitihada za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi ambapo kwasasa Tanzania inafanya mapitio ya kanuni za usimamizi wa kemikali zinazo momonyoa tabaka la ozoni za mwaka 2007.

Waziri huyo alisema hadi sasa jitihada za utekelezaji wa mikataba ya kulinda tabaka la ozoni, kumechangia kupungua kwa kiasi cha asilimia 98, takribani tani milioni 1.8 ya uzalishaji na matumizi ya kemikali zinazomomonyoa tabaka hilo.



Meneja wa Vodacom Tanzania Foundation, Sandra Oswald akizungumza wakati wa maadhimisho ya miaka 35 ya uhifadhi wa tabaka la ozoni yaliyoandaliwa na Ofisi ya Makamu wa Rais, jijini Dodoma jana. Kampuni hiyo, imetoa vifaa na kompyuta zenye thamani ya zaidi ya sh milioni 13 kwa ajili ya zawadi kwa washindi wa kitaifa wa shindano la kuandika insha. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Moto wa kampeni za Mavunde washika kasi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MGOMBEA ubunge wa Jimbo la Dodoma Mjini kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Anthony Mavunde, ameendelea kuchanja mbuga katika kampeni zake huku akiahidi mambo mbalimbali.

Miongoni mwa mambo aliyoahidi ni kukuza kilimo cha zabibu kwa kutafuta masoko na uhakika pindi akichaguliwa tena kuwa mbunge wa jimbo hilo.

Akizungumza jana katika mkutano wa kampeni kata ya Mpunguzi ambayo ni maarufu kwa kilimo cha zabibu, Mavunde alisema kama atachaguliwa, atatafuta masoko na kuwawezesha kinamama na vijana kuchakata zabibu na kuuza mchuzi wa zabibu. "Ili kuondokana na zabibu kuoza mashambani nikichaguliwa nitahakikisha nawawezesha vijana na kinamama kuchakata na kuuza mchuzi wa zabibu, kama mnavyojua zabibu yetu inasifika kimataifa kutokana na ubora wake, hivyo kuchakata kutaongeza tija kwenye kilimo hiki, na itakuwa faida kwa wakulima," alisema.

Aidha, alisema atahakikisha anawawezesha wakulima wa nyanya kupata mikopo, ili kuongeza tija kwenye uzalishaji na uchakataji wa nyanya. Kuhusu ujenzi wa shule, Mavunde aliahidi kukamilisha ujenzi wa shule ya sekondari mpya ya Nkulabi iliyoanza kujengwa na yeye akishirikiana na wananchi mwaka jana alipokuwa mbunge wa jimbo hilo.

"Pia mkinichagua tutaanza ujenzi wa shule ya msingi mpya eneo la Mlangwa ili kupunguza kero ya wanafunzi kutembea umbali mrefu kufuata elimu," alisema.

Kadhalika, alisema katika sekta ya maji na umeme atakamilisha miundombinu ya miradi ya maji Mpunguzi B na Nkulabi na kusimamia usambazaji wa umeme katika maeneo machache yaliyosalia.

"Nitaendelea kukuza michezo na sanaa kwa kufadhili mashindano mbalimbali kwa lengo la kukuza vipaji," alisema.

## Waandaa tamasha kumpongeza JPM

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

UMOJA wa Vijana Wazalendo nchini, umejipanga kufanya tamasha la kumpongeza Rais John Magufuli kwa mafanikio yaliyofikiwa kwa kipindi cha miaka mitano ya utawala wake.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma, Mratibu wa tamasha hilo, Simon Mwapagata, maarufu kama Rado, alisema tamasha hilo litafanyika kwa siku tatu mfululizo kuanzia Oktoba 22 hadi 24, mwaka huu.

Mwapagata alisema linatarajiwa kuwakutanisha watu kutoka makundi mbalimbali, ambayo yamepata mafanikio kwenye serikali ya awamu ya tano.

"Hili suala si la kisiasa bali ni uzalendo wetu sisi vijana ambao tumeona tumpongeze Rais wetu kwa mafanikio makubwa tuliyoyapata kwenye uongozi wake wa miaka mitano," alisema na kubainisha kuwa tamasha hilo limepewa jina la karibu Dodoma Festival.

"Tanzania haijawahi kusimama hata siku moja si wakati wa ugonjwa wa corona na hata sasa wakati wa kampeni nchi haijasimama shughuli zinaendelea kama kawaida, hivyo tamasha hili lisihusishwe na masuala ya kisiasa," alisema.

Alitaja watu watakaoshiriki kwenye makundi ya bodaboda, mama lishe, machinga, watu wenye ulemavu, wanafunzi wa vyuo, wanafunzi wa shule za sekondari na msingi, vijana, wanawake, wazee, wafungwa walio huru na waathirika wa dawa za kulevya.

Katibu wa Jumuiya ya wenye Ulemavu Tanzania, John Mlabu, alisema watu wenye ulemavu watashiriki katika tamasha hilo ili kumpongeza Rais Magufuli kutokana na serikali ya awamu ya tano kutenga asilimia mbili ya mapato ya halmashauri kwa ajili ya mikopo kwa watu hao.

Alisema watu wengi wenye ulemavu wamechangamkia fursa hiyo na wamefanikiwa kuendesha shughuli zao za kila siku na kuachana na kuomba omba mitaani.

Naye Mwakilishi wa kundi la wanawake katika tamasha hilo, Mariam Fentu, alisema wanawake wamefanya shughuli zao bila kubughudhiwa na mtu yeyote kutokana na kuwapatia vitambulisho vya wajasiriamali.





## Mgombea ajinadi kuboresha elimu

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

MGOMBEA udiwani Kata ya Kisiba, wilayani Rungwe kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Ambakisye Mwakanyamale, ameahidi kuwa endapo atapata ridhaa ya kuiongoza kata hiyo, atahakikisha anaboresha mazingira ya elimu.

Katika kufanya hivyo amesema atahamasisha ujenzi wa shule za msingi na sekondari. Pia amesema atasimamia ujenzi wa kituo cha afya na zahanati ili kusogeza karibu huduma za kijamii kwa wananchi.

Mwakanyamale aliyasema hayo juzi wakati wa mkutano wa kampeni zake uliofanyika kwenye viwanja vya Kisina na kueleza ahadi zote alizozitoa lazima azitimize kwa kuwa amejipima na ameona anafaa kuwaongoza wana Kisiba.

Alisema ili wananchi wapate maendeleo ya haraka na uhakika, ni lazima wamchague kiongozi ambaye atayashughulikia matatizo yao kwa namna yoyote ama kwa kuyafikisha kwa viongozi au yeye binafsi kutatua.

"Naijua vizuri Kata ya Kisiba pamoja na vitongoji vyake juu ya matatizo yanayowakabili. Tunahitaji kiongozi ambaye atashughulikia sekta za afya, elimu na mikopo, lakini mazingira wezeshi kwa watu wenye ulemavu," alisema.

Mwakanyamale alisema baadhi ya vikwazo vinavyowakabili wakazi wa Kisiba ni miundombinu ya barabara, ukosefu wa maji safi na salama, umeme kwa baadhi ya vitongoji, ujenzi wa vyumba vya madarasa na fursa za kupitia kilimo cha ndizi na parachichi.

Baadhi ya wananchi, akiwamo Abraham Mwaipopo, walisema imekuwa kawaida kwa baadhi ya madiwani pindi wanapopata ridhaa ya kuongoza husahau majukumu yao kama walivyoahidi na kukwamisha miradi mbalimbali ya maendeleo.

Walisema kutokana na mazingira hayo, imesababisha wananchi kutokuwa na imani kwa wagombea na badala yake hulazimika kusikiliza sera na kuhoji endapo wanayoyaahidi watayatimiza.

"Kila mgombea wa udiwani anatuahidi mambo mazuri kweli ya kuyatekeleza na sisi huwa tuaamini. Sasa umefika wakati tunashindwa kumtambua yupi mkweli na mwongo maana baadhi ya wenzetu wanashindwa kupiga kura. Ukiangalia kata yetu haina barabara nzuri, maji ni shida baadhi ya vitongoji havina umeme huu ni mwaka wa nane sasa,"alisema Mwaipopo.

Alisema hitaji lao ni kumpata kiongozi ambaye atakubali kubeba matatizo ya wananchi ya kwenda kuyasemea kwa viongozi kupitia vikao mbalimbali vya uamuzi.

# Utata waibuka wodi kuungua moto

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

UTATA umeibuka kuhusu chanzo cha moto ulioteketeza wodi ya wazazi ya Hospitali ya Wilaya ya Kyela baada ya kubainika kuwa jengo hilo halijawahi kuwekewa miundombinu ya umeme na halikuwahi kutumika kwa shughuli zozote zinazohusiana na moto.

Moto huo uliibuka mwishoni mwa wiki iliyopita wakati baadhi ya wagonjwa wakiwa wamelazwa na kuteketeza baadhi ya mali zilizokuwamo kama vitanda na dawa huku wagonjwa wakiokolewa bila kudhurika.

Akizungumza juzi baada ya kutembelea na kushuhudia athari za moto huo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, aliliagiza Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola, kufanya uchunguzi wa kina ili kubaini chanzo halisi. Chalamila alisema kutokana na jengo hilo kutokuwa na umeme wala miundombinu ya umeme, ana uhakika taarifa itakayotolewa na vyombo hivyo haitahusisha kabisa mambo ya nishati hiyo na badala yake watakuja na kitu kingine.

"Inawezekana wakachelewa kuleta taarifa kwa sababu yapo mambo mengi ya kuchunguza. Lakini kiufupi ni kwamba jengo halijawahi kufanyiwa 'wiring' (kutandazwa nyaya za umeme)," alisema Chalamila.

Alisema katika ajali hiyo hakuna dawa zilizoungua isipokuwa vitanda vilivyokuwamo viliteketea na akaahidi kuwa serikali itavinunua na kuvipeleka haraka ili wagonjwa waendelee kupata huduma.

Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Cloudia Kitta, alisema mbali na athari za uharibifu wa jengo na miundombinu mingine iliyokuwamo, pia athari zilitokea kwa wagonjwa waliokuwa wamelazwa kwa kuokolewa na watu wasiokuwa na utaalamu.

Alisema baadhi ya wagonjwa waliokuwa wamelazwa ndani ya jengo hilo walikuwa wametundikiwa dripu za maji, hivyo wakati wa kuokolewa walitolewa bila kuzingatia taratibu za kitaalamu, lakini wagonjwa wote wako salama.

"Kwa kuwa lilikuwa ni tukio la ghafla, wako vijana ambao walijitolea kuja kuokoa na hivyo walilazimika kuwatoa wagonjwa dripu hizo bila utaalamu wowote na jambo la kumshukuru Mungu ni kwamba wagonjwa wetu wako salama," alisema Kitta.

Alisema baada ya wagonjwa hao ambao walikuwa tisa kuokolewa ndani ya wodi hiyo, walihamishiwa katika Kituo cha Afya cha Ipinda ambako wanaendelea na matibabu mpaka sasa na afya zao zinaendelea kuimarika.




Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Philip Mangula (katikati), akiwa pamoja na wagombea ubunge wa majimbo yote ya Mkoa wa Mbeya juzi, alipokuwa akihitimisha ziara ya siku tisa kwenye majimbo hayo na kukabidhi gari maalumu (nyuma yao), itakayotumika kwenye kampeni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mangula: CCM ni dereva mzoefu inastahili kuendelea kuongoza nchi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Philip Mangula, amewataka wakazi wa Mkoa wa Mbeya kuwachagua wagombea wa chama hicho kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka huu akidai chama hicho kina uzoefu wa kuongoza nchi.

Mangula ambaye ni mlezi wa CCM Mkoa wa Mbeya, aliyasema hayo juzi alipokuwa anahitimisha ziara yake ya siku tisa kwenye majimbo yote ya mkoa kwa ajili ya kukagua maandalizi ya chama kuelekea uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu.

Mbali na kukagua maandalizi ya chama, pia aliukabidhi uongozi wa CCM mkoa gari maalumu ambalo litakuwa linatumika kwenye kampeni za wabunge kwenye majimbo yote ya mkoa.

Alisema kwachagua wagombea wa vyama vya upinzani ni sawa na kumpa dereva anayejifunza aendeshe gari zuri na la bei kubwa akitolea mfano gari aina ya Land Cruiser V8.

Kwa mujibu wa Mangula, kwenye ziara yake aliridhishwa na maandalizi kwenye majimbo yote, hivyo ana uhakika kuwa chama hicho kitapata ushindi mkubwa kuliko ilivyokuwa mwaka 2015.

"Sisi ni madereva wenye leseni ya daraja la kwanza na tunaenda kuwaomba wananchi 'tu-renew' (kuhuisha) leseni yetu. Sasa huwezi kumpa 'leaner' (dereva anayejifunza) aendeshe gari hili zuri ambalo ni nchi yetu. Nawaomba Watanzania watuamini kwa sababu tumefanya makubwa," alisema Mangula. Alisema kwenye uchaguzi wa mwaka 2015, wananchi wa Mkoa wa Mbeya walimuunga mkono Rais John Magufuli kwa asilimia 53 na kwamba kwa kazi alizozifanya katika kipindi cha miaka mitano, ataungwa mkono kwa asilimia zaidi ya 90.

Gari lililokabidhi, alisema lilitolewa na baadhi ya watu wanaokipenda chama hicho na kwamba yeye pamoja na kuwa ndiye mlezi wa chama, hana uwezo wa kulinunua kwa maelezo kuwa linauzwa kwa bei kubwa.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa, Mchungaji Jacob Mwakasole, alisema katika uchaguzi wa mwaka 2015, chama kilipoteza jimbo moja kati ya saba ya mkoa huo.

Alisema jimbo hilo ni la Mbeya Mjini, ambalo lilichukuliwa na Joseph Mbilinyi 'Sugu' ambaye ameliongoza kwa miaka 10 na anawania awamu ya tatu.

Mwakasole alisema kwa sasa chama kimejipanga kuhakikisha kinanyakua majimbo yote likiwamo la Mbeya Mjini kwa kumng'oa Sugu.

Alisema gari ambalo alikabidhiwa na Mangula litawasaidia kuongeza nguvu kwenye kampeni ili wawashinde majimbo yote.

"Nikuhakikishie kwamba nyenzo hii ni muhimu na itatusaidia sana kuwashughulikia majirani. Naamini kuwa ingekuwa mpira wa miguu wangetamani kuomba wasiingie uwanjani," alisema Mwakasole.



# Mwinyi aahidi kujenga kiwanda cha mwani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGOMBEA urais wa Zanzibar kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Hussein Mwinyi, amewahakikisha wakulima wa mwani kuwajengea kiwanda ili kufaidika na zao hilo iwapo atapata ridhaa ya kuwa Rais wa Zanzibar.

Aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na wananchi wa kijiji cha Paje Mkoa wa Kusini Unguja ikiwa ni sehemu ya kampeni zake za kuomba nafasi hiyo.

Dk. Mwinyi aliwahakikishia wakulima wa zao hilo kuwajengea kiwanda kama kilichokuwapo kisiwani Pemba, ili kujiendeleza kimaisha na kujipatia maendeleo.

Alisema pia atawawezesha wakulima wa zao hilo kupata taaluma ya ukulima bora, kilimo hicho ambacho wahusika wengi ni wanawake. Pia alisema serikali atakayoiongoza, iwapo atachaguliwa, lazima iweke nguvu kubwa kwa zao hilo kwa kuwa ndiyo sehemu inayoajiri watu wengi.

Dk. Mwinyi aliipongeza serikali ya awamu ya saba kwa kazi nzuri iliyofanywa katika utekelezaji wa ilani ya kupeleka huduma mbalimbali kwa wananchi zikiwamo umeme na maji na kuahidi serikali ya awamu ya nane chini ya CCM itamalizia pale palipobakia.

"Unapotaka kujenga uchumi mpya lazima uwe na miundombinu bora ya barabara na majengo ya kisasa ambayo (Rais) Dk. (Ali Mohamed) Shein ameanza nami naahidi nitamalizia," alissema.

Aidha, alisema atawasaidia watu wanaotaka kujenga viwanda vidogo vya kusarifu matunda ili kuwawezesha watu kupata ajira na soko la bidhaa zao.

Dk. Mwinyi alisema serikali atakayoiongoza itaangalia upya mifumo ya kodi na baadhi ya kodi ambazo ni kero kwa wananchi zitaunganishwa ili wananchi wasipate usumbufu.

Kadhalika, alisema pia serikali atakayoiongoza itawatambua rasmi wafanyabiashara wa bodaboda ili kuwawezesha kutambulika kisheria.

Dk. Mwinyi alisema biashara ya bodaboda ni ajira ambayo inamwezesha mwananchi kupata kipato cha kujiendesha kimaisha, hivyo hakuna sababu ya kutotambulika na kutokuwa katika mfumo rasmi.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akishiriki dua iliyosomwa na Mufti Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Omar Saleh Kabi, baada ya kumaliza kuusalia mwili wa marehemu Salim Hassan Abdallah Turky, iliofanyika katika Masjid Noor Mohammad Kwamchina, jijini Zanzibar juzi. Kulia kwake ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi na (kushoto kwake), mtoto wa marehemu Tofiq Salim Turky, Naibu Kadhi Mkuu wa Zanzibar Sheikh Hassan Othman Ngwali na Makamu wa Rais mstaafu, Dk. Mohammed Gharib Bilal na mgombea urais wa Zanzibar kupitia CCM, Dk. Hussein Mwinyi (kulia). **PICHA: IKULU**

# Wakulima, wavuvi walia mazingira magumu

**Na Rahma Suleiman,** PEMBA

WAVUVI na wakulima wa mwani wa Tumbe kisiwani Pemba, wamesema wanafanya kazi hiyo katika mazingira magumu ambayo baadhi yao husababisha kufariki dunia.

Waliyaeleza hayo juzi wakati walipotembelewa na mgombea urais wa Zanzibar kupitia ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, aliyefika kijiji hapo kwa ajili ya kuomba kura.

Masoud Abdallah Mwinyi ni miongoni mwa wavuvi wa kijiji hicho, alisema wavuvi wengi kijijini hapo wanapoteza maisha kwa sababu vyombo wanavyovulia ni vidogo.

"Tunakomba Maalim Seif ukiwa rais au kama una mpango wowote tufanyie ili tupate boti za kisasa za uvuvi na za uokozi ambazo zitatufaa sisi na wakulima wa mwani," alisema Mwinyi kwa niaba ya wavuvi wenzake.

Naye mkulima wa mwani, zao ambalo hulimwa baharini, Halima Ali, alisema hata wao baadhi yao hufariki dunia baharini kutokana kina kikubwa cha maji na hawana zana za kisasa za kuendeleza kilimo hicho.

Alisema wamekuwa wakipoteza nguvu kazi kutokana na kulima mwani kwenye maji mengi kwa kutumia vyombo vidogo vya baharini ambavyo haviwezi kuhimili mawimbi makubwa ya bahari. "Licha ya kwenda mbali na kina kikubwa cha maji, bei hii haituridhishi hata kidogo. Nyonga zote zimekufa kwa kuinama muda mrefu wakati bei ya mwani ni ndogo," alisema mkulima huyo.

Kutokana na kilimo hicho, Maalim Seif alisema atakapoingia madarakani atahakikisha wavuvi wanakopeshwa boti za bei nafuu ili kuvua katika maji makubwa na kuwa salama.

Alisema atahakikish wavuvi wote wanakuwa na mawasiliano na wanamaji ili likitokea tatizo waweze kufanya mawasiliano ya haraka na kuokoa maisha yao.

"Tunakusudia kuyabadilisha maisha ya Wazanzibar kwa muda mfupi bila kuwabaguwa watu kwa sababu ya vyama vya siasa au dini," alieleza Maalim Seif.

Akizungumdia zao la mwani, alisema katika serikali yake atahakikisha anaongeza bei ya mwani kutoka Sh. 600 hadi Sh. 1,000 kwa kilo na kuwapatia vifaa vyote ambavyo vitarahisisha katika kazi zao.

Mgombea huyo pia alisema endapo wananchi wa Zanzibar watamchagua, atahakikisha wakulima wa mwani wanapata faida kwa kuweka bei nzuri ambayo itakidhi machungu ya kilimo hicho. Alieleza wanunuzi wa mwani wanawadhulumu wakulima kwa kununua zao hilo kwa bei ya chini ya Sh. 600 kwa kilo moja.

## Serikali kuwaunga mkono wanaharakati

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mkoa wa Mjini Magharibi imesema itaendelea kushirikiana na kusaidia wanaharakati na makundi mbalimbali ya kijamii katika kuhamasisha na kutoa elimu kuhusu amani na utulivu wakati wa nchi ikielekea kwenye uchaguzi mkuu.

Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi, Hassan Khatib Hassan, alisema hayo katika kongamano maalum la uzinduzi wa uhamasishaji amani na utulivu katika kipindi cha kuelekea uchaguzi mkuu lililoandaliwa na taasisi ya wasanii wa filamu lililofanyika Forodhani Mjini Unguja.

Alisema Zanzibar ni visiwa vya amani hivyo ni vyema kila mmoja akatimiza wajibu wake wa kusimamia na kuitunza amani iliyopo hususani kipindi hiki taifa likikabiliwa na uchaguzi.

"Ule msemo wa mtoto akililia wembe mpe mimi siupendi. Nasema mtoto akililia wembe uficha maana ukimkata wewe uliyemwachia ndiye utakayeathirika, hivyo amani si kitu cha kukichezea. Ikitoweka wengi tutaathirika," alisema Hassan.

Mkuu huyo wa mkoa aliupongeza uongozi wa taasisi ya wasanii wa filamu Zanzibar kwa kuaandaa mpango huo wa kuhamasisha amani na kuyataka makundi mengine kushirikiana hiyo katika kufanikisha mpango huo.

Naye Naibu Mkurugenzi wa Mipango na Uchaguzi wa CUF, Mohammed Vuai Makame, alisema chama chao kitahakikisha kinakuwa mstari wa mbele katika kuona amani ya nchi inadumu muda wote kabla na baada ya uchaguzi mkuu.

"Sisi viongozi na wanachama wa CUF tutahakikisha tunahamasisha amani na utulivu muda wote kabla na baada ya uchaguzi maana uchaguzi ni siku moja lakini miaka mitano tunatakiwa tufanye kazi za maendeleo ili kujiimarisha kiuchumi," alisema Mohammed.

Nao baadhi ya wasanii na wanaharakati waliiomba serikali ya mkoa kuwasaidia katika kuwajengea uwezo ili kutumia ushawishi walio nao katika jamii kuhamasisha suala la amani na utulivu katika maeneo mbalimbali.

Mratibu wa mpango huo wa utoaji wa elimu ya amani kutoka taasisi ya wasanii wa filamu Zanzibar, Ahmed Harith, alisema taasisi hiyo imekusudia kupita maeneo mbalimbali ya Zanzibar zikiwamo shule na vyuo kuelimisha jamii umuhimu wa amani kupitia sanaa zao.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL**
Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile:

- Kuboresha biashara
- Kulipa kodi ya nyumba
- Kumalizia tenda
- Kulipa matibabu n.k.

Mawasiliano yetu: Dar es salaam **– 0768 928 516. Arusha – 0677 226 960.**

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA (SAMMONS)**
**(MCA/63)**

**Mahakama ya Mwanzo ya ARUSHA**
**Wilaya ya ARUSHA**

**Madai Nambari 194/2020**

**MDAI HAMISI YUSUPH MALESA**

**Dhidi ya**

**MDAIWA MWIDINI SALIMU**
**Kwa kuwa mdai/Wadaiwa ameleta/wameleta madai yake/yao ya (eleza aina ya madai hapa chini)**
**Madai 194/2020**

Kwa hiyo unahitaji/mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya tarehe 21-09-2020 saa 08:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo. Fika na hati zako zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya utetezi wako kama upo.

Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu endapo mahakama itathibitisha umepokea/mmepokea kuitwa shaurini hii itaweza kutoa HUKUMU kuwa umeshindwa /mmeshindwa kesi.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 14-09-2020

21-09-2020 14-09-2020

**Hakimu/Hakimu Mkazi / Mahakama ya Mwanzo.**

115903802

## KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI

**EDWINI MHAGAMA** wa mjini Geita, anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaji yake yenye namba za usajili **MC. 877 CBG.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu yake. Taarifa ya Polisi. Polisi Taarifa: **GE/TR/RB/428/2020.**

115903302

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**Shamimu Shabani Kimaro** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **RAV 4** yenye namba ya usajili **T761 DGQ** iliyotolewa na Mamlaka ya mapato Tanzania. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/MAG/RB/670968/2020**

115904002

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**Gladness Raymond Lema** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA PREMIO** yenye namba ya usajili **T829 BWM** iliyotolewa na Mamlaka ya mapato Tanzania. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/MAG/RB/672055/2020**

115904302

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**Ndugu Stephania John Mutalemwa** amepotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 856 BFC,** cheassis namba **MD2A18AZ3GWK38892** na injini namba **DUZWGK42150** aina ya Boxer Ametoa taarifa polisi na kupewa RB No. **KAG/BUK/RB/654881/2020.** Kwa yeyote atakayeiona apige simu namba **0769-227636.**

115904202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No; 271/2020**

**Ombi la SHOMARI RASHIDI,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu RASHID MISEMBE.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 28/09/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 15/09/2020.

Tarehe 15/9/2020

Sahihi ya Hakimu
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

115904402

**Uza,**

**Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza**

**Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuzi kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Wagundua viumbe sayari ya Venus

**LONDON, Uingereza**

WATAALAMU wa angani wamegundua viumbe wanaoishi kwa kuelea katika mawingu ya sayari ya Venus.

Phosphine ni kitu chenye sumu na chenye harufu mbaya walichokigundua katika mawingu hayo ya sayari ya Venus na ambacho kinaonekana kuwa ishara ya uhai katika sayari hiyo.

Duniani, Phosphine inahusishwa na uhai, inapatikana katika viumbe vidogo vinavyoishi katika koo za wanyama kama vile pingu ama maeneo yenye mazingira duni ya hewa kama vile vidimbwi vya maji ardhini. Ni gesi inayoweza kuzalishwa katika viwanda.

Hivyo basi tunauliza ni kwa nini gesi hii ipo yapata kilomita 50 kutoka ardhini?

Prof. Jane Greaves wa Chuo Kikuu cha Cardiff na wenzake wanauliza swali kama hilo.

Na wamechapisha taarifa katika jarida la asili ya anga zinazoelezea ugunduzi wao kuhusu Phosphine katika sayari ya Venus, pamoja na uchunguzi waliofanya ili kujaribu kuonesha kwamba molekyuli hiyo inaweza kuwa na chanzo asilia na kisicho cha kibaiolojia. Lakini kwa sasa wamechanganyikiwa.

Juu ya kila kitu kinachojulikana kuhusu sayari, hakuna aliyefanikiwa kuelezea chanzo cha Phosphine kibaiolojia.

Hii ina maana kwamba ni vyema kugundua kwamba kuna ishara za uhai katika sayari hiyo.

"Tangu nianze kazi yangu nimekuwa na hamu kujua iwapo kuna uhai katika maeneo mengine ya ulimwengu, hivyo nafurahi kwamba hilo linawezekana," Prof. Greaves alisema.

Lakini ni kweli tunawashinikiza watu wengine kutuambia kile ambacho huenda tumekosa. Stakabadhi zetu pamoja na takwimu ziko wazi, hivyo ndivyo jinsi sayansi inavyofanya kazi.

Sayari ya Venus haipo katika orodha ya uwezekano wa uhai katika maeneo mengine ya mfumo wa sayari, ikilinganishwa na dunia ni jahanam.

Asilimia 96 ya anga yake ina gesi ya kaboni, kiwango cha joto katika sakafu yake ni zaidi ya nyuzi 400.

Vifaa vya angani vilivyotua katika sayari hiyo vimechukua dakika chache kabla ya kuharibika.

Hata hivyo, umbali wa kilomita 50 Kaskazini, viwango vya joto siyo vya juu.

Hii ndiyo sababu inaaminika kwamba iwapo kuna uhai katika sayari ya Venus basi ni katika eneo hili.

Mawingu yake ni mazito na yanamiliki kati ya asilimia 75 hadi 95 za tindi kali ya Sulphuric, ambayo ni hatari kwa viumbe vinavyoishi duniani.

*BBC*



Rais wa Halmashauri Kuu ya Ulaya, Ursula von der Leyen, akihutubia Bunge la Ulaya, na kuhimiza umoja kujenga muungano imara wa afya. **PICHA: MTANDAO**

# Suga Waziri Mkuu mpya Japan

**TOKYO, Japan**

BUNGE la Japan limemchagua, Yoshihide Suga, kuwa Waziri Mkuu mpya wa nchi hiyo, baada ya Shinzo Abe kujiuzulu.

Baada ya kushinda uongozi wa chama tawala mapema wiki hii, kura zilizopigwa jana zimeidhinisha rasmi wadhifa wa mkuu huyo zamani wa mawaziri.

Waziri mkuu huyo mpya ambaye ni mshirika wa karibu wa Abe, anatarajiwa kuendeleza sera ya mtangulizi wake.

Abe alitangaza kujiuzulu mwezi uliopita kutokana na sababu za afya.

Jumatano, Abe alifanya mkutano wake wa mwisho wa mawaziri na kuwaambia wanahabari kwamba anajivunia utawala wake wa karibu miaka minane.

Suga alishinda kirahisi katika uchaguzi wa Waziri Mkuu katika Bunge la Diet, ambalo ni la chini nchini Japan, baada ya kupata kura 314 kati ya 462 zilizopigwa

Ushindi wake ulitarajiwa na wengi, ikizingatiwa kwamba muungano unaoongozwa na chama chake cha Liberal Democratic Party (LDP), una wabunge wengi.

Suga pamoja na mawaziri wake wapya baadaye wataidhinishwa rasmi katika hafla itakayoandaliwa katika Imperial Palace.

*BBC*

# ECOWAS yatamani utawala wa kiraia Mali

**ACCRA, Ghana**

RAIS wa Ghana, Nana Akufo-Addo, amesema viongozi wa Magharibi mwa Afrika wana matumaini ya kuiona serikali inayoongozwa na raia ikiwekwa nchini Mali katika kipindi cha siku kadhaa.

Akufo-Addo aliyazungumza hayo baada ya mazungumzo baina ya viongozi wa kikanda na wanamgambo wa Junta ambao walichukua mamlaka nchini mali mwezi uliopita.

Alisema kuwa jumuiya ya kiuchumi ya nchi zilizoko magharibi mwa Afrika ECOWAS, wataondoa vikwazo mara moja pale raia watakapochukua mamlaka nchini Mali.

Viongozi wa ECOWAS walikutana katika mji mkuu wa Ghana, Accra, kwa mazungumzo kuhusu mzozo wa kisiasa wa Mali.

Viongozi wa Jeshi la Mali Junta, Kanali Assimi Goita, pamoja na wawakilishi kutoka Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika pia walihudhuria.

Viongozi wa mataifa ya Afrika Magharibi wanahofia kwamba hali ya usalama nchini Mali inaweza kuharibiwa zaidi na kudhoofishwa kwa juhudi zilizofanyika kuyashinda makundi ya wapiganaji wa kiislamu.

Jumamosi, upinzani unaofahamika kama M5-RFP ulipinga pendekezo la jeshi la mchakato wa kipindi cha mpito cha miezi 18.

**BBC**

# Watuhumiwa 32 kundi la uhalifu kizimbani

**KIGALI, Rwanda**

WATU 32 wamefikishwa mahakamani nchini Rwanda kwa tuhuma za kuwa wapiganaji wa kundi la Rwanda National Congress (RNC) linaloendesha harakati zake Mashariki mwa Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Baadhi yao wanaongozwa na Meja mstaafu wa Jeshi la Rwanda, Habib Mudathiru na wengine wakiwa askari watoro kutoka Jeshi la Rwanda.

Wanashtakiwa kujiunga na wapiganaji wa kundi la RNC ambalo linaongozwa na Mkuu wa zamani wa Majeshi ya Rwanda anayeishi uhamishoni nchini Afrika Kusini, Jenerali Kayumba Nyamwasa.

Wapo wengine waliojiunga na wapiganaji wa vuguvugu la P5 ambalo pia linaendesha harakati zake Mashariki mwa DRC.

Wote walikamatwa katika mapigano mashariki mwa Congo mwaka jana na baadaye kukabidhiwa Rwanda.

Watuhumiwa wengi wanakiri mashtaka dhidi yao na kusema kwamba waliingizwa katika makundi hayo kwa nguvu.

**BBC**

# NEYMAR

## KUFUNGIWA MECHI NNE LIGUE 1




**PARIS, Ufaransa**

NEYMAR anakabiliwa na kufungiwa mechi nne kwa kumpiga Alvaro Gonzalez, baada ya kumtuhumu mlinzi huyo wa Marseille kwa kumtolea maneno ya ubaguzi wa rangi, kwa mujibu wa winga wa zamani wa Paris Saint-Germain, Jerome Rothen.

Nyota huyo wa kimataifa wa Brazil alikuwa mmoja wa wachezaji watano walitolewa nje kwa kadi nyekundu kwenye mchezo wa Jumapili uliomalizika kwa vurugu kubwa wakati Marseille ikiibuka na ushindi wa bao 1-0 pale Parc des Princes.

VAR ilionyesha kwamba Neymar akimpiga Alvaro ngumi nyuma ya kichwa, huku mshambuliaji huyo akisema sababu ya kufanya hivyo ni kutokana na kutolewa maneno ya ubaguzi wa rangi.

PSG na Marseille kila moja imewatetea wachezaji wake na sasa wanasubiri maamuzi ya Bodi ya Ligi Kuu ya Ufaransa, ambayo ilifanyia uchunguzi tukio la vurugu hizo kwenye mchezo huo.

Maamuzi yalitarajiwa kutolewa jana Jumatano na Rothen anatarajia Neymar kupigwa adhabu ya kufungiwa mechi.

"Kwa Neymar, anaweza kufungiwa mechi nne, nina uhakika na hilo," alisema akiiambia RMC Sport.

"Niliwahi kupigana baada ya mechi uwanjani na nikafungiwa mechi nne."


PSG pia iliwapoteza Leandro Paredes na Layvin Kurzawa ambao nao walionyeshwa kadi nyekundu, huku Jordan Amavi na Dario Benedetto wa Marseille nao walilimwa kadi nyekundu.

PSG ambao ni mabingwa watetezi wa Ligue 1 na walitinga fainali ya Ligi ya Mabingwa msimu uliopita, walianza msimu huu wa 2020-21 kwa kufungwa mechi mbili mfululizo, ikiwamo dhidi ya Lens.

Kikosi hicho cha kocha, Thomas Tuchel jana Jumatano kilitarajiwa kucheza na Metz, kabla ya kwenda kuwavaa Nice, Reims na Angers ndani ya siku 16 zijazo.

# Grealish asaini miaka mitano

**LONDON, England**




JACK Grealish amesaini mkataba mpya wa miaka mitano na Aston Villa na hivyo kumaliza uvumi wa kwamba anaondoka klabuni hapo na kwenda Manchester United.

Villa ilitangaza kumsainisha mkataba huo mpya Grealish kupitia kwenye tovuti yao na sasa ataichezea klabu yake hiyo ya utotoni hadi mwaka 2025.

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 25, ambaye alianza kwa mara ya kwanza kuichezea timu ya Taifa ya England dhidi ya Denmark mwezi huu, kwa mara ya kwanza alitamba kwenye Ligi Kuu msimu wa 2014-15 na 2015-16, wakati bado akiwa kijana.

Alibakia na timu hiyo baada ya kushuka daraja, licha ya kupata ofa za klabu kubwa na msimu uliopita aliisaidia kubaki kwenye Ligi Kuu.

Msimu uliopita alifunga mabao nane na kutoa pasi za mwisho sita kweye Ligi Kuu na kuwa na mchango mkubwa kwa kikosi hicho.

Kwa upande wake, Grealish amesema: "Nina furaha kubwa kuendelea kubakia hapa Villa. Ni klabu yangu, ni nyumbani kwangu na nina furaha kubwa hapa."

# Bale anataka kurudi Spurs, asema wakala

**LONDON, England**

RAGETH Bale anaweza kwenda Tottenham Hotspur baada ya wakala wa nyota huyo wa Real Madrid kubainisha kuwa anataka kurudi katika klabu hiyo.

Bale mchezaji wa kimataifa wa Wales amekuwa hana nafasi pale Madrid chini ya kocha, Zinedine Zidane, licha ya kuisaidia klabu hiyo kutwaa mataji matatu ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 31, alifurahia wakati mzuri alipojiunga na Madrid kutoka Spurs, Septemba 2013 kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia kwa wakati huo ya euro milioni 100.

Tottenham imeripotiwa kuwa katika mazungumzo ya kutaka kumsajili tena Bale, huku ikionekana kama anaweza kujiunga kwa mkopo lakini mshahara wake wa pauni 600,000 kwa wiki unaonekana kuwa mgumu kuufikia.

Hata hivyo, wakala wa winga huyo, Jonathan Barnett amebainisha kwamba anataka kurudi tena kuichezea klabu hiyo ya London Kaskazini.

"Gareth bado anaipenda Spurs," alisema akiiambia BBC Sport Wales. "Ni sehemu anayotaka kwenda."

Manchester United mara kwa mara imekuwa ikihusishwa na Bale kwa kipindi ambacho amekuwa akicheza kule LaLiga.



MAKALA




Mshindi wa kwanza mwanamke aliyetajirika kwa kubeti kupitia Jackpot ya SportPesa, Scolastika Ngwalueson, akikabidhiwa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 260.3 Oktoba mwaka jana na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi SportPesa, Tarimba Abbas nyumbani kwao Chamanzi jijini Dar es Salaam. **PICHA: MAKTABA**

# KUBETI
## Mchezo wa uhakika unaotajirisha wengi haraka

**Na Adam Fungamwango**

TOFAUTI na miaka iliyopita ambapo wachezaji wa michezo ya kubashiri hofu na mashaka ilikuwa imetawala kuhusu upangaji wa matokeo, mambo yamebadilika kabisa katika mchezo wa kubashiri matokeo ya michezo mbalimbali, maarufu kama 'kubeti'.

Kumekuwa na ongezeko kubwa sana la wachezaji wa mchezo wa kubeti nchini Tanzania kwa sasa ambapo kuna kampuni nyingi zinazoendesha biashara hiyo, halali ambayo imekuwa chanzo kikubwa cha mapato serikalini huku Watanzania wa rika mbalimbali vijana kwa wazee wakizidi kutajirika kupitia mchezo huo.

Hii inatokana kwanza kabisa na mazingira yenyewe ambayo yamekuwa yakiboreshwa mara kwa mara. Ikumbukwe wakati michezo ya kubashiri matokeo ya inaingia inchini, mfumo mmoja tu ndiyo ulikuwa unatumika.

Nao ni ule wa kujaza kwenye makaratasi tu. Mpaka leo bado upo na watu wanaendelea kubeti, lakini kwa sasa umebaki kuwa wa vijana zaidi, huku marika mengine yakibashiri zaidi kupitia mitandao ya simu na intaneti.

Vijana wamekuwa wakijitokeza kwenye kumbi za kubeti wakitafuta bahati yao na kweli, wengine wao wametajirika, na kutoboa kwenye maisha yao, wanaume kwa wanawake, hii yote ikitokana na uhakika wa kulipwa na kujua mshindi wa kweli.

Mfumo wa kutumia simu za mkononi na hata teknolojia ya kubeti kwenye mitandao, hii imefanya watu wengi zaidi kwenye nyadhifa mbalimbali, na hata wafanyakazi wa maofisini kubeti kwa wingi ambapo awali walikuwa wanashindwa kutokana na kutokuwa na muda wa kwenda kwenye kumbi zilizojengwa maalum kwa shughuli hiyo.

Kampuni za kubeti nchini, SportPesa Tanzania, M-Beti, Premier Beti, Sokabeti, Parimatch na mengineyo kwa sasa zimekuwa zikinufaika mno na mfumo huo kwani sasa watu wanabeti kwa njia rahisi ya mtandao popote pale walipo, nyumbani, kwenye vyombo vya usafiri, ofisini na kwingineko.

### Uhakika

Tukirudi kwenye kubeti kwenyewe ni kwamba, hivi sasa hakuna mtu yeyote ambaye ana wasiwasi na hilo, kwani wengi wamekuwa wakipata pesa kila wanaposhinda.

Kampuni za kubetisha michezo mbalimbali zimekuwa zikiwalipa washindi mara tu mechi zinapomalizika na wala hakuna longolongo huku serikali ikipata kodi yake papo hapo, jambo ambalo linaongeza imani kwa wachezaji.

Hali hii imewafanya hata wale waliokuwa wakihofia kubahatisha, nao kuanza kucheza kila wanapopata nafasi hiyo. Michezo ya kubashiri hasa mechi mbalimbali za michezo duniani imeendelea kujipatia umaarufu na kuvutia wengi kwa sababu ni ya uwazi zaidi, kuliko michezo mingine ambayo hata ukijua vigezo vinavyotumika kumpata mshindi, bado kuamini inakuwa ni vigumu.

Kwenye kubeti ni mtu mwenyewe anaamua timu fulani itashinda na nyingine itafungwa na inapotokea hivyo, wala haihitaji kutagazwa mshindi, kwani aliyecheza mwenyewe anatambua kuwa ameshinda. Kizuri zaidi ni kupata pesa yake ya ushindi baada ya muda mfupi tu.

**Lakini kinachofurahisha zaidi ni uwapo wa vipengele vingi vya kucheza, kwani unaweza kuchagua nani anafunga, mabao mangapi, kona ngapi, faulo ngapi, matokeo ya jumla hadi kadi za njano na nyekundu, hivyo mwisho wa mchezo unajua wazi umeshinda ama la.**

Hii imewasaidia watu wengi kutajirika kwa kubeti. Wengine wamekuwa wakipata pesa ambazo zimekuwa zikiwaongezea kipato chao, licha ya kazi na biashara wanazofanya.

Mkurugenzi wa Utawala na Uendeshaji wa SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas, hapa anakumbusha washindi walioibuka na utajiri mkubwa kwa kushinda dau kubwa katika Jackpot ya SportPesa.

"Agosti 2019 tulipata washindi wawili waliopata kila mmoja zaidi ya Sh. milioni 414, kisha mwezi mmoja baadaye tukapata mshindi wa kwanza wa Jackpot mwanamke aliyeshinda zaidi ya Sh. milioni 260, Scolastica Ngwalueson, pia Februari 2020, mshindi mwingine alishinda zaidi ya Sh. milioni 437, huku Julai mwaka huu akipatikana mshindi wa Sh. milioni 288.9 kwenye Jackpot," alifafanua Tarimba namna Watanzania wanavyonufaika wanaume kwa wanawake.

Kwa uhakika mchezo wa kubeti unatengeneza mabilionea wengi nchini kwa sasa, huku masharti na vigezo vyote vikifuata na waendeshaji wa michezo hiyo nchini.

Lakini pia sote tunakuwa mashahidi kwa namna ambavyo kambuni hizo zimekuwa zikijitokeza kuinua sekta ya michezo nchini na kuinua uchumi wa jamii, mfano mzuri ni mabilioni ya shilingi ambayo SportPesa Tanzania imetumia kuzidhamini klabu za Simba, Yanga, Namungo na awali Singida United.

Si hilo tu, ubora wa Uwanja wa Mkapa, kina mtu anaushuhudia kwa sasa baada ya SportPesa Tanzania kutumia kiasi kikubwa cha fedha kukarabati eneo la kuchezea 'pitch' huku pia Watanzania wakinufaika kwa kuziona klabu kubwa barani Ulaya ikiwamo Everton, Sevilla zikicheza katika ardhi ya Tanzania.

Kwa upande wa jamii tumeona namna vijana wengi walivyowezeshwa kujiajiri wenyewe kupitia Bajaj imara za TVS Kings Delux baada ya kubashiri kupitia kampuni hiyo.

Lakini pia kujitoa kwa SportPesa kumehamasisha kampuni nyingine kujitokeza kusaidia sekta ya michezo ambapo mwaka huu tumeshuhudia Kampuni ya Kubashiri Matokeo ya Parimatch ikiingia mkataba wa mwaka mmoja wa kuidhamini Klabu ya Mbeya City wenye thamani ya Shilingi milioni 270.

Hata hivyo, kampuni ya kubeti inasisitiza jinsi ya kucheza michezo hiyo kwa kufuata sheria na taratibu za nchi, huku wanaotakiwa kucheza wakiwa ni wale wenye umri kuanzia miaka 18.

Inawezekana pia kuna watu wanaotaka kuanza kubeti, lakini hawaelewi waanze vipi kutokana na kutojua sana mambo ya michezo, elimu hiyo pia imekuwa ikitolewa kwa weledi kabisa na kampuni hizo.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# AUBAMEYANG ATOA SABABU KUSAINI MI3

Kusaini mkataba mpya na klabu hii kamwe haikuwa shaka kwangu, tuna kitu fulani cha kuvutia hapa na...

**LONDON, England**

PIERRE-Emerick Aubameyang amemaliza uvumi juu ya majaliwa yake baada ya kusaini mkataba mpya wa miaka mitatu na Arsenal, huku akiaeleza kilichomsukuma kufanya hivyo niimani yake ya kufanya makubwa na klabu hiyo.

Nahodha wa 'Washikabunduki' hao mkataba wake wa mwanzo ulikuwa unamalizika Juni mwakani, lakini amekubali kusaini mpya na klabu hiyo ya Ligi Kuu ya England.

Straika Aubameyang amefunga mabao 72 katika mechi 111 tangu ajiunge na Arsenal kutoka Borussia Dortmund kwa ada ya pauni milioni 56 Januari mwaka 2018.

"Kusaini mkataba mpya na klabu hii kamwe haikuwa shaka kwangu," alisema Aubameyang akiiambia tovuti ya Arsenal.

"Nawashukuru mashabiki wetu, wachezaji wenzangu, familia yangu na kila mmoja klabuni hapa kwani najiona ni sehemu ya klabu hii.

"Naiamini Arsenal. Tunaweza kufanikiwa kwa mambo makubwa pamoja. Tuna kitu fulani cha kuvutia hapa na naamini mambo mazuri zaidi yanakuja kwa Arsenal."

Katika msimu wake wa kwanza hapo Arsenal wa 2018-19, Aubameyang alifunga mabao 22 na kutwaa Kiatu cha Dhababu.

Msimu uliopita nyota huyo mwenye umri wa miaka 31, alifurahia mafanikio mengi akifunga mabao 29 katika mechi 44 alizocheza katika mashindano yote.

Alifunga kwenye nusu fainali ya Kombe la FA dhidi ya Manchester City na Chelsea na pia alifunga penalti ya ushindi pale kwenye dimba la Wembley katika mchezo wa Ngao ya Jamii dhidi ya Liverpool.

Arsenal ilianza msimu mpya wa Ligi Kuu kwa ushindi wa 3-0 dhidi ya Fulham pale kwenye dimba la Craven Cottage, ambako Aubameyang alifunga bao la tatu wakiwa wanacheza ugenini nyumbani kwa West Ham, Jumamosi iliyopita.

## KWA UFUPI

**DELE ALLI CHAMBO YA BALE**

KLABU ya Tottenham Hotspur huenda wakamtumia kiungo wa kati wa England, Dele Alli mwenye umri wa miaka 24, kama chambo wakati wakijaribu kumrejesha Gareth Bale mwenye miaka 31 kutoka Real Madrid. ***(Mail)***

**EVERTON KUWAUZA WALCOTT, IWOBI**

EVERTON inaweza kukubali ofa za kuwanuza wachezaji wake, Theo Walcott mwenye umri wa miaka 31, winga wa Nigeria, Alex Iwobi mwenye miaka 24 na mshambuliaji, Moise Kean ambaye ana miaka 20, wakati wakitarajia kukiongezea nguvu kikosi cha Carlo Ancelotti. ***(Mirror)***

**ARSENAL KUONGEZA WACHEZAJI**

ARSENAL bado wanapanga kuwaongeza wachezaji zaidi kwenye kikosi chao, huku wakiwalenga kiungo wa kati wa Atletico Madrid, Thomas Partey mwenye umri wa miaka 27 na kiungo mchezeshaji wa Lyon, Mfaransa Houssem Aouar mwenye miaka 22. ***(Mirror)***

**BAYERN WAMRUDIA HUDSON-ODOI**

BAYERN Munich wako tayari kurudisha shauku yao kwa winga Callum Hudson-Odoi mwenye umri wa miaka 19, huku wababe hao wa Ligi ya Mabingwa Ulaya wakiwa na matumaini kuwa Chelsea itapokea ofa yao. ***(Mail)***

**BARCELONA WAMTAKA GRACIA**

KLABU ya Barcelona itajaribu kumsajili mlinzi wa Manchester City, Eric Garcia mwenye umri wa miaka 19, kama wataweza kuwauza Samuel Umtiti mwenye miaka 26 na Jean-Clair Todibo, 20. ***(Mail)***

**ARSENAL WAKOMAA NA PARTEY**

KIUNGO wa kati wa Atletico Madrid, Thomas Partey ni miongoni mwa wachezaji wanaotolewa macho na Arsenal wakitaka kumsajili. ***(Mail)***

**JUVE HATIHATI KUMKOSA SUAREZ**

KLABU ya Juventus wanakumbana na wakati mgumu kuhusu kumsajili mshambuliaji wa Barcelona, Luis Suarez, ambaye anapata changamoto kupata pasi ya Italia kwa haraka.***(Goal)***

**CHELSEA YAKARIBIA KWA MENDY**

CHELSEA inakaribia kukamilisha taratibu za kumsajili nyota wa kimataifa wa Senegal, Edouard Mendy mwenye umri wa miaka 28. ***(Star)***

**INTER INASHAWISHI PALMEIRI**

INTER Milan bado wanamshawishi kumpa mkataba wa kudumu beki wa Chelsea, Emerson Palmieri mwenye umri wa miaka 26, lakini West Ham pia inamtolea macho wakitaka akachezee kikosi hicho kwa mkopo. ***(Independent)***

**ROMA KUACHANA NA SMALLING**

KUSHINDWA AS Roma kukubaliana na Manchester United kuhusu ada ili kumpata beki wa kati, Chris Smalling kutaifanya klabu hiyo ya Italia kufikiria kuhusu mbadala. ***(Mail)***

**ARSENAL YAIGOMEA SHEFFIELD**

ARSENAL imekataa ombi la Sheffield kumnyakua mshambuliaji, Folarin Balogun. Klabu hiyo inaaminika kutoa ofa ya pauni milioni 3 na marupurupu mengine, lakini 'Washikabunduki' hao wanataka dili ya karibu pauni milioni 15 kwa ajili ya mchezaji huyo mwenye miaka 19, ambaye amechezea vikosi vya vijana vya Marekani na England. ***(Mail)***



HABARI MICHEZO

# HAT-TRICK ZATABIRIWA KWA BOCCO, SARPONG 2020/21

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa zamani wa Pamba ya Mwanza na Yanga, Fumo Felician, amewatabiria wachezaji, John Bocco wa Simba, Mghana Michael Sarpong wa Yanga pamoja na Obrey Chirwa wa Azam FC, kufunga magoli matatu kwenye mechi moja 'hat-trick' kama watakuwa kwenye viwango vyao, walivyovionyesha katika mechi za awali.

Fumo, aliyesifika enzi zake kwa mashuti makali, alisema anapenda Ligi Kuu msimu huu ilivyoanza, kwani inaonekana timu zote zimejidhatiti, lakini anaona ni ya muda tu, kwani mbele ya safari timu zitajigawa kama kawaida na zile zenye wachezaji wazuri na vikosi vipana, ndizo zitakazofanya vizuri.

"Na niseme tu inaonekana kama vile mabao hayapatikani sana, lakini kwangu naona huko mbele yatafungwa mengi sana na wachezaji kama Bocco, Sarpong na Chirwa, jinsi nilivyowaona kwenye mechi hizi, watafunga sana, tena kuna mechi watafunga hat-trick," alisema mchezaji huyo wa zamani.

Alisema pamoja na ushindani mkubwa unaoonekana, lakini kuna timu ambazo hazina vikosi kwenye wachezaji wengi wazuri, hivyo baadaye ligi itagawanyika kwa timu zinazosaka ubingwa, kubaki Ligi Kuu na kupigania kushuka daraja.

Kumekuwa na maoni mbalimbali ya wadau wa Ligi Kuu baada ya raundi mbili za awali, baadhi wakionekana kufurahishwa na upinzani mkali ulioonyeshwa na timu zote 18, zile zilizoshinda zikionekana kushinda kwa mbinde, na hata zilizofungwa zikionekana kupambana na kupoteza mechi kwa mbinde.

KWA SAMATTA...




Kipa Muargentina Emiliano Martinez, akionyesha jezi ya Aston Villa aliyokabidhiwa baada ya kusaini mkataba wa miaka minne kwa dau la pauni milioni 16 akitokea Arsenal alikodumu kwa miaka 10. Klabu hiyo ndiyo anayoichezea nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samatta. **PICHA: MTANDAO**

# Mshindi wa pili Ligi Kuu sasa kucheza CAF

**Na Adam Fungamwango**

BODI ya Ligi Kuu Tanzania Bara, imerekebisha baadhi ya kanuni msimu huu na sasa mshindi wa pili wa ligi atacheza michuano ya Shirikisho barani Afrika (CAF), kama bingwa wa Ligi Kuu ndiye atakayetwaa pia Kombe la FA.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi hiyo, Almas Kasongo, alisema jijini Dar es Salaam jana kuwa, pamoja na kanuni nyingine zilizorekebishwa, kanuni hiyo imepitishwa, ili kuipa thamani Ligi Kuu, lakini kuleta ushindani kwenye michuano ya Kombe la FA.

"Tulitoa nafasi kwa wadau wote wa michezo kuleta mapendekezo ya mabadiliko ya kanuni, na moja ya mabadiliko hayo ni kurekebisha hii ya mshindi wa pili wa Ligi Kuu, kucheza Kombe la Shirikisho Afrika, kama ikitokea bingwa wa Ligi Kuu akachukua tena Kombe la FA," alisema Kasongo.

Alisema kanuni hii imerekebishwa, ili kuleta ushindani kwenye Ligi Kuu na Kombe la FA pia.

Alisema baada ya kutafakari na kuangalia yaliyotokea, hasa kwenye mechi ya fainali ya Kombe la FA, Simba ikicheza dhidi ya Namungo, wakati tayari zote zikiwa zimeshakata tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa, kanuni hiyo ilionekana inahitajika.

Kutokana na mabadiliko hayo, timu yoyote sasa itakayofika fainali ya Kombe la FA na ikafungwa na timu ambayo pia imetwaa ubingwa, haitoshiriki michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, kama ilivyokuwa kwa Namungo mwaka huu dhidi ya Simba, badala yake timu itakayoshika nafasi ya pili kwenye ligi tu ndiyo itakayoshiriki michuano hiyo.

Hata hivyo, bingwa wa Kombe la FA bado ataendelea kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Ikumbukuwe kuwa, bingwa wa Tanzania anaiwakilisha nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, hivyo hata ikitwaa tena Kombe la FA haiwezi kushiriki michuano hiyo.

## KCB yaimwagia Ligi Kuu mil. 500/-

**Na Saada Akida**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limeingia mkataba wa mwaka mmoja wenye thamani ya Sh. milioni 500 za Kitanzania na Benki ya KCB, kwa ajili ya kuongeza nguvu katika msimu wa 2020/21 wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini jana, Makamu wa Pili wa Rais TFF, ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Ligi nchini (TPLB), Steven Mguto, alisema wameingia mkataba kwa awamu ya nne kwa kiasi hicho cha fedha, ambacho wanakiongeza katika mapungufu na sehemu nyingine kukielekeza katika matumizi ya ligi msimu huu.

Alisema huu ni mwaka wa nne wanaingia mkataba na fedha hizo, wataongezea katika sehemu ambayo kutakuwa na mapungufu.

"TFF na Bodi ya Ligi tunafurahi kuona wadau wanajitokeza kusapoti soka la Tanzania, wana imani na sisi na udhamini huo, utaendelea kuleta hamasa na ushindani mkubwa katika ligi yetu," alisema.

Naye Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa KCM, Barry Chale, alisema wanaendelea kuwa miongoni mwa wadhamini wa ligi baada ya kuthamini sekta ya michezo, ambayo sasa imekuwa ajira kubwa nchini.

## Mwadui yatamba kuisimamisha KMC

**Na Adam Nyangasa, TUDARCo**

LICHA ya kuanza vibaya kwa kupoteza michezo miwili ya mwanzo ya Ligi Kuu Bara, Kocha Mkuu wa Mwadui FC, Khalid Adam, amesema hana shaka ya kufanya vizuri katika mechi yao ijayo dhidi ya vinara wa ligi hiyo, KMC FC ya jijini Dar es Salaam.

Mwadui FC, ambayo Jumatatu ijayo itaikaribisha KMC FC katika Uwanja wa CCM Kambarage mjini Shinyanga, imeanza msimu huu kwa kupoteza bao kwa 1-0, dhidi ya Dodoma Jiji, ugenini kabla ya kupokea tena kipigo kama hicho nyumbani kwa Biashara United ya Musoma.

Lakini akizungumza na gazeti hili jana, Adam alisema kikosi chao kipo 'fiti' na kinaendelea na mazoezi na hana majeruhi ya kutisha kikosini yanayoweza kumtia hofu ya kufanya vizuri katika mchezo huo, ambao utakuwa wa kwanza kwao kucheza nyumbani msimu huu.

**"Ninaiheshimu KMC FC ni timu ngumu, pia imeanza ligi vizuri msimu huu, lakini hatutakuwa waoga kwa matokeo ya wapinzani wetu, sisi pia tuna mipango yetu na tumejipanga kwa ajili ya kuchukua pointi tatu muhimu kwenye mchezo huo.**

"Uwanja wetu tumeuzoea na tunafanya mazoezi kila siku, kwa kuzingatia hilo, wachezaji wangu itakuwa ni rahisi na ukizingatia mechi ni saa nane mchana na hali ya hewa ya Shinyanga tumeizoea, nyumbani ni nyumbani na kuna kila sababu ya sisi kufanya vizuri," alisema kocha huyo.

Michezo
Alhamisi Septemba 17, 2020
Nipashe



AUBAMEYANG ATOA SABABU KUSAINI MI3 HABARI UK 22

# SIMBA YAONYWA STRAIKA MMOJA

**Na Adam Fungamwango**

KIPA wa zamani wa Simba, Steven Nemes, ameonya kuwa timu hiyo ikiendelea kutumia straika mmoja, itapata tabu sana kupata ushindi kwenye mechi zake za Ligi Kuu Tanzania Bara, badala yake inatakiwa itumie mastraika wawili.

Nemes ambaye kabla ya kuhamia Simba alikuwa akiichezea Yanga, alisema kuwa Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck anafanya makosa kumchezesha straika mmoja mbele jambo ambalo anaifanya timu yake kupata tabu sana ya kushinda, kwa sababu tayari baadhi ya makocha wameshagundua mbinu yake.

"Kwanza kabisa kuchezesha straika mmoja ni lazima awe na uwezo mkubwa wa kumiliki mpira na kukaa nao kwa sekunde kadhaa, mwenye nguvu ya kuweza kukabiliana na mabeki wawili au watatu wa timu pinzani, na pia asiwe anatoka sana kwenye eneo la goli kwenda kutafuta mpira sehemu nyingine," alisema Nemes.

Aliongeza kuwa Bocco, pamoja na kuwa na sifa ya kukaa na mpira na nguvu, lakini ana tabia ya kutoka kwenda nyuma, kati na pembeni, hivyo eneo la kati linakuwa halina mtu, hivyo safu hiyo ya ushambuliaji inapwaya.

"Kama Bocco akiwa na Kagere, basi mmoja anatoka kwenda pembeni au kati, lakini mmoja anabaki eneo la hatari na hii huwa inawasaidia sana Simba kupata ushindi tena wa mabao mengi, lakini hii ya straika mmoja inakuwa na matatizo kwa sababu, hata viungo ambao wamewekwa ili wamsaidie kumlisha straika mmoja, nao bado hawafanyi kazi yao vizuri, hilo ni tatizo," alisema.

Nemes pia alisema kwenye mechi za mikoani ambako viwanja si vizuri sana ndiyo tatizo linakuwa kubwa zaidi, hivyo angalau awe hivyo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, lakini viwanja vya mikoani straika mmoja ni tatizo zaidi kutokana na staili ya ucheza wa Simba, hivyo kumtaka kocha huyo abadilike kama anataka kutetea ubingwa wao.

TUNAJIFUA...



Kiungo Carlos Carlinhos (kushoto) na Tuisila Kisinda wakiwa mazoezini pamoja na wachezaji wenzao wa Yanga. Timu hiyo itasafiri leo kuelekea Bukoba tayari kwa mechi yao ya raundi ya tatu ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Kagera Sugar, itakayopigwa Jumamosi katika Uwanja wa Kaitaba mjini humo. **MPIGAPICHA WETU**

# ZLATKO: CARLINHOS BADO NI WA BENCHI YANGA SC

## ●●●Amjumuisha pia Yacouba, asema anaendelea kutafuta ubora wao hadi hapo...

**Na Saada Akida**

LICHA ya kiungo Carlos Carlinhos, kuchangia ushindi ndani ya dakika 29 alizoichezea Yanga dhidi ya Mbeya City Jumapili iliyopita katika Uwanja wa Mkapa jijini Dar es Salaam, huo ukiwa ni mchezo wake wa kwanza wa Ligi Kuu tangu ajiunge na klabu hiyo msimu huu, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Zlatko Krmpotic amesema bado benchi linamhusu Muangola huyo.

Katika mchezo huo ambao Yanga ilishinda bao 1-0, Carlinhos aliingia akitokea benchi dakika ya 61 kuchukua nafasi ya Feisal Salum 'Fei Toto', ambapo mbali na mashuti yake mawili kushindwa kujaa nyavuni, kona yake ya dakika ya 86 kutoka wingi wa kushoto, iliunganishwa kimyani kwa kichwa na beki wa kati, Mghana Lamine Moro.

Kiwango hicho kimewafanya mashabiki kupitia vyombo mbalimbali vya habari na mitandao ya kijamii kupaza sauti zao wakimtaka Zlatko kuanza kumwanzisha katika kikosi cha kwanza ili kuisaidia timu kupata ushindi.

Lakini Zlatko amesema wachezaji Carlinhos na mshambuliaji Yacouba Sogne, na baadhi yao ataendelea kuwapa dakika chache za katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara hadi hapo watakapokuwa fiti kama anavyohitaji.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Zlatko alisema nyota hao walionyesha mabadiliko makubwa na kucheza vizuri, lakini ataendelea kuwapa dakika chache iwe za mwanzo au mwisho za kucheza hadi watakapokuwa fiti.

Alisema kutocheza kwa miezi minne hadi mitano katika nchi walizotoka kutokana na janga la corona lililoikumba dunia, analazimika kuwapa dakika chache za kucheza ili miili yao iwe tayari kuhimili kucheza kwa dakika nyingi.

"Miezi minne hadi mitano kwa mchezaji bila kucheza ni mingi sana, Carlinhos na Yocouba ni wachezaji wazuri na wana uwezo mkubwa wa kusaidia timu kupata matokeo, lakini bado hawajawa fiti zaidi ili kunishawishi kuwapa muda mrefu wa kucheza," alisema Zlakto ambaye ni raia wa Serbia.

Alisema mashabiki wanatakiwa kuvumilia pamoja na kuwaamini wachezaji wao kwa sababu anaendelea kusuka kikosi cha timu hiyo kuweza kupata matokeo mazuri katika mechi zake.

Kocha huyo alisema ataendelea kuwapa nafasi ya kucheza kila mchezaji kwa ajili ya kuwaweka fiti zaidi ya walivyocheza katika mechi iliyopita dhidi ya Mbeya City.

"Kuna wachezaji ambao wameonyesha muunganiko mzuri kwa sababu walianza kufanya mazoezi mapema, waliochelewa naendelea kuwapa dakika chache za kucheza," alisema Zlatko ambaye amerithi mikoba ya Luc Eymael aliyetimuliwa mwishoni mwa msimu uliomalizika.

Alisema maandalizi yao dhidi ya Kagera Sugar yanaendelea vizuri, na lengo lao ni kuhakikisha wanapata matokeo mazuri katika mchezo huo utakaopigwa Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba Jumamosi.

Kikosi cha Yanga kinatarajiwa kuondoka jijini Dar es Salaam leo kuelekea Kagera tayari kwa mchezo huo wa raundi ya tatu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >